# KUCHUNGUZA DHIMA ZA NYISO ZA JAMII YA KIUYU MAAMBANI

**ZUHURA SAID MOHAMED**

**TASINIFU ILIYOWASILSHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A. KISWAHILI FASIHI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini, anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo: *Kuchunguza Dhima za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani*, na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa shahada ya Uzamili (M.A Kiswahili) katika Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

………………………………………..

**Dkt. Felistas Richard Mahonge**

**(Msimamizi)**

Tarehe………………………

# HAKIMILIKI

Tasnifu hii ni mali yangu binafsi, hivyo hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote kama, kielektroniki, kurudufu nakala au kurekodi bila ya ithibati ya mwandishi au ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, **ZUHUR SAID MUHAMED,** nathibitisha kuwa kazi hii niliifanya mimi mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyengine yoyote.

**Saini**……………………………….

**Tarehe .........................................**

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii, kwanza kwa wazazi wangu wapendwa bibi na babu ambao ni bwana Yussuf Ali Khamis na bi Maryam Hamad Bakar kwa kunipa malezi mema na zaidi kwa kunipeleka shule na kunipatia elimu tangu shule ya awali hadi leo nakamilisha shahada ya uzamili mchango wao ni mkubwa sana. Mwenyenzi Mungu awape malipo mema Duniani na Akhera. Amin.

Pili, natabaruku kazi yangu kwa muume wangu mpenzi Bw. Mbarouk Mussa Mbarouk kwa kunihamasisha kuendelea na masomo yangu, mchango wake ulinisaidia sana katika kukamilisha masomo yangu ya Uzamili.

Tatu naitabaruku kazi hii kwa watoto wangu Nasra Mbarouk Mussa, Mussa Mbarouk Mussa, Abdurahman Mbarouk Mussa, Mahmuod Mbarouk Mussa, Husna Mbarouk Mussa, Abdulhafidh Mbarouk Mussa na Hafsa Mbarouk Mussa na nawaombea kwa Mungu awaongoze katika misingi ya elimu na dini.

## SHUKURANI

Awali ya yote napenda kumshuru Mwenyezi Mungu Subhanallahu Wataala kwa kunijaalia uhai pamoja na afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu pamoja na kunipa maarifa ambayo nimeyatumia katika muda wote wa masomo ya shahada ya Uzamili. Ninasema Alhamdulilahi.

Pili, napenda kumshukuru kwa moyo wa dhati msimamizi wangu Dkt. Felistas Richard Mahonge kwa kunipa ushauri na kuniongoza hatua kwa hatua hadi tasnifuu hii kukamilika. Sina la kumlipa ispokuwa na muomba Mwenyezi Mungu ampe kila la kheri. Dkt. Naahidi kwamba mchango wako sitousahau katika tathnia hii ya elimu hadi naingizwa kaburini.

Tatu, napenda kuwashukuru wazazi wangu bibi Maryam Hamad Bakar na bwana Yussuf Ali ambao ndio walionilea na kunisomesha ili kupata maarifa ambayo ninayatumia hadi sasa. Aidha, shukurani za pekee nazitoa kwa muume wangu mpenzi Bwana Mbarouk Mussa Mbarouk pamoja na watoto wangu Nasra Mbarouk Mussa, Mussa Mbarouk Mussa, Abdurahman Mbarouk Mussa, Mahmuod mbarouk Mussa, Husna Mbarouk Mussa, Abdulhafidh Mbarouk Mussa na Hafsa Mbarouk Mussa kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu pamoja na kunitia moyo ili kufanikisha kazi hii.

Nne, kwa sababu kukamilika kwa kazi hii ni pamoja na mchango na ushauri wa watu wengi ambao kuwataja wote isingekuwa rahisi, hata hivyo, hapa ningependa kuwataja wachache ambao ni pamoja na mwalimu Bw. Bakari Kombo Bakari, mwalimu Nassor Ali Sleman, mwalimu Amour Rashid Ali kwa msaada wao pamoja na ushauri ambao uliwezesha kazi hii kukamilika. Allah awape afya njema na kila la kheri.

## IKISIRI

Utafiti huu umechunguza *Dhima za Nyimbo za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani*. Utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo ni:- Kubainisha nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani, Kueleza dhamira zinazojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani na Kufafanua dhima za nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani. Utafiti huu ulikuwa ni wa uwandani ambapo data zake zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili. Mtafiti alifanya usaili na wanawake 20 wa Kiuyu Maambani ambao wamewahi kuhudhuria mafunzo ya unyago ambayo yanaambatana na nyiso. Jumla ya nyimbo 30 zilikusanywa na baadae mtafiti aliteua nyimbo 17 ili kutumika kuwa sampuli ya utafiti huu. Data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Vile vile, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa kwa kutumia kigezo cha dhima, nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaweza kuwekwa katika makundi ya nyimbo zinazofunza usafi, nyimbo zinazokuza umoja na mshikamano, nyimbo zenye kuonya, nyimbo zenye kuhamasisha kazi, nyimbo zinazofunza maisha ya ndoa na nyimbo zinazoendeleza utamaduni wa jamii. Dhamira zinazopatikana katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ni za utamaduni, mapenzi na ndoa, usafi, uaminifu katika ndoa, kuondoa woga, umoja na mshikamano na dhamira ya kazi." Matokeo ya utafiti huu yameonesha pia kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima za kukuza mshikamano katika jamii, kuhimiza ustahamilivu, kubainisha utamaduni wa jamii, kuhimiza ujasiri amali, kufundisha maadili mema na kuburudisha. Mwisho, utafiti unahitimisha kwamba nyimbo za ngoma ya nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ni muhimu sana katika kuwafanya wanawake kuwa na maadili bora ya maisha yao ya ndoa na jamii kwa ujumla.

**Maneno Makuu:** *Nyiso, Nyimbo, Dhima*

# YALIYOMO

UTHIBITISHO .......... ii

HAKIMILIKI .......... iii

TAMKO .......... iv

TABARUKU .......... v

SHUKURANI .......... vi

IKISIRI .......... vii

YALIYOMO .......... viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA .......... 1**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Mada .......... 1

1.3 Tatizo la Utafiti .......... 4

1.4 Lengo la Utafiti .......... 5

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .......... 5

1.4.2 Madhumuni Mahasusi .......... 5

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 6

1.7 Mipaka ya Utafiti .......... 6

1.8 Muundo wa Tasnifu .......... 7

**SURAYA PILI:UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA .......... 8**

2.1 Utangulizi .......... 8

2.2 Ufafanuzi wa Dhana .......... 8

2.2.1 Maana ya Nyimbo ........ 8
2.2.2 Jando ........ 10
2.2.3 Unyago ........ 10
2.2.4 Dhamira ........ 11
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Nyimbo ........ 12
2.3.1 Tafiti Kuhusu Nyimbo ........ 13
2.3.2 Tafiti Kuhusu Dhima za Nyimbo ........ 14
2.4 Pengo la Utafiti ........ 19
2.5 Mkabala wa Kinadharia ........ 20
2.5.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ........ 20
2.6 Hitimisho ........ 23

**SURA YA TATU: BINU ZA UTAFITI ........ 25**

3.1 Utangulizi ........ 25
3.2 Umbo la Utafiti ........ 25
3.3 Eneo la Utafiti ........ 25
3.4 Walengwa wa Utafiti ........ 26
3.5 Sampuli na Usampulishaji ........ 26
3.5.1 Sampuli ........ 26
3.5.2 Usampulishaji ........ 27
3.6 Data za Utafiti ........ 28
3.6.1 Data za Msingi ........ 28
3.6.2 Data za Upili ........ 28
3.7 Mbinu za Kukusanya Data ........ 29

3.7.1 Mbinu ya Usaili ........................................................................ 29
3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka ........................................................ 30
3.8 Uchambuzi wa Data ........................................................................ 30
3.9 Hitimisho ........................................................................................ 31

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZIWA DATA ZA UTAFITI ........................................................................ 32**

4.0 Utangulizi ........................................................................................ 32
4.1 Nyimbo za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani ................................ 32
4.1.1 Nyimbo Zinazofunza Usafi ............................................................ 32
4.1.2 Nyimbo zinazokuza Umoja na Mshikamano .................................. 34
4.1.3 Nyimbo Zenye Kuonya ................................................................... 34
4.1.4 Nyimbo za Kuhamasisha Kazi ........................................................ 35
4.1.5 Nyimbo Zinazofunza Maisha ya Ndoa ............................................ 36
4.1.6 Nyimbo Zinazoendeleza Utamaduni ............................................... 37
4.2 Dhamira za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani ............................... 39
4.2.1 Utamaduni ...................................................................................... 39
4.2.2 Mapenzi na Ndoa ........................................................................... 43
4.2.3 Usafi ............................................................................................... 46
4.2.4 Uaminifu katika Ndoa ..................................................................... 48
4.2.5 Kuondoa Woga ............................................................................... 49
4.2.6 Umoja na Mshikamano ................................................................... 51
4.2.7 Umuhimu wa Kazi .......................................................................... 52
4.3 Dhima Katika Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani ............................ 54

4.3.1 Kukuza Mshikamano katia Jamii ........ 54
4.3.2 Kuhimiza Ustahamilivu ........ 55
4.3.3 Kubainisha Utamaduni wa Jamii ........ 58
4.3.4 Kuhimiza Ujasiriamali ........ 62
4.3.5 Kufundisha Maadili Mema ........ 63
4.3.6 Kuburudisha ........ 66
4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 67

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 68**

5.1 Utangulizi ........ 68
5.2 Muhutasari wa Tasinifu ........ 68
5.3 Matokeo ya Utafiti ........ 70
5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 70
5.3.2 Lengo Mahsusi la Pili ........ 70
5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu ........ 71
5.4 Hitimisho ........ 71
5.5 Mapendekezo ........ 71
5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine ........ 71
5.5.2 Mapendekezo kwa Wanajamii ........ 72

**MAREJELEO ........ 73**

**VIAMBATISHO ........ 77**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sehemu hii ni sehemu ya utangulizi ambayo imewasilisha vipengele muhimu vya kiutangulizi ambavyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu hii.

## 1.2 Usuli wa Mada

Waziri (2016) anaeleza kuwa katika jamii nyingi za Afrika watu hufanya sherehe mbalimbali kama vile za jando, unyago, mwakakogwa, miviga nakadhalika. Sherehe hizo huambatana na nyimbo ambazo huwa na dhima katika jamii kama vile kuburudisha, kuonya, kuwatayarisha vijana kuanza maisha mapya, kutunza historia mila na desturi za jamii nakadhalika.

Nyiso ambazo huwa ni nyimbo za jando na unyago ni miongoni mwa nyimbo maarufu katika makabila mbalimbali. Nyimbo hizi huimbwa katika shughuli za miviga (Mulokozi, 1996). Katika jamii za Uswahilini, nyiso huimbiwa wari wakati watoto hao wanapovunja ungo na wakati wa sherehe ya harusi. Kwa sababu miviga ni suala la utamaduni kama zilivyo tanzu nyengine za sanaa ya maonesho zimekuwa zikirithiwa toka kizazi hadi kizazi.

Katika kueleza sanaa ya miviga Muhando na Balisidya (1976) wanaeleza kuwa miviga ni sanaa ya maonesho ambayo hujumuisha jando na unyago. Lengo la miviga ni kumuingiza mtu toka kundi fulani kwenda kundi jengine. Kundi linaloelezwa hapa ni lile la utoto kwenda kwenye kundi la watu wazima. Hivyo kwa upande wa nyimbo za nyiso wanazoimbiwa watoto wa kike zinahusu mambo muhimu katika maisha yao.

Kwa mujibu wa Mzee (2016) anaeleza kwamba dhima za nyiso ni kumtoa kijana kutoka kundi la watoto na kuingia katika kundi la watu wazima. Pili, ni kumfundisha yale yote yahusianayo na utu uzima kama vile umuhimu wa kazi, ushonaji, umuhimu wa kuwa na ujasiri na nafasi ya mtu katika suala zima la ulinzi wa jamii nzima. Tatu, nyimbo huwafundisha watoto suala la unyumba na malezi bora ya watoto.

Naye Mulokozi (1996) anasema kuwa nyiso ni nyimbo za unyago. Nyimbo hizi huimbwa na jamii zenye mila ya kupeleka watoto unyagoni. Nyiso kwa kawaida hukusudiwa kuwaasa wari kuhusu majukumu yao mapya ya utu uzima pindi watakapohitimu jando au unyago. Maelezo haya ya Mulokozi yanatupa uelewa kwamba nyimbo za nyiso hupatikana katika miktadha ya unyago. Pia, tumepata uelewa kwamba mafunzo makuu ya nyimbo za nyiso huhusu kumtayarisha kijana kuwa tayari kubeba ama kukabiliana na yale yote wanayofanya watu wazima katika jamii husika.

Tafiti kadhaa zimewahi kufanywa zikijikita kuchunguza nyimbo. Mathalan, Moh`d (2015) alichunguza dhima za nyimbo za msondo wa jamii ya Wapemba. Katika utafiti huo aligundua kuwa nyimbo za msondo katika jamii ya Wapemba zina dhima ya kuelimisha, kuburudisha, kuwafunza wanandoa na kadhalika.

Vile vile, Rashid (2013) alifanya utafiti wenye mada ya utafiti "*Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi.*" Utafiti huo uligundua kuwa jamii ya Wahiyao wanatumia jando na unyago kama sehemu ya kuonesha utajiri na ufukara wao kutokana na hali zao za maisha. Vijana wanaowekwa jandoni na unyagoni ni wa umri mdogo kati ya miaka 2-5. Rashid anasema kwamba kwa sababu ya umri wao mdogo hawawezi kutunza mafunzo ya

jando na unyago. Athari yake ni kwamba watoto hao hukosa mafunzo imara na hatimae ni kujiingiza katika uvunjifu wa maadili ikiwemo kushiriki katika uasharati na hivyo kupata mimba za nje ya ndoa.

Naye Mzee (2016) alifanya utafiti uliohusu kuchunguza nyimbo za singo ambazo ni nyimbo wanazoimbiwa wanawake wakati wa kufundishwa usafi wa mwili wanapokuwa kwenye unyago katika kijiji cha Uzini Unguja. Katika utafiti huo anaeleza kuwa wapo wanajamii wanaoamini kwamba nyimbo hizo za singo zimekuwa zikikiuka maadili na zimekuwa zikitumiwa na watu wasiokuwa na ustaarabu. Hata hivyo utafiti wa Mzee ulionesha kuwa nyimbo za singo hufundisha mwanamwari taaluma inayofaa ya kukabiliana na maisha yake ya ndoa, kuwatimizia waume haki zao, kujenga moyo wa subira katika kukabiliana na matatizo, kuishi vizuri na majirani, kuepuka uhusiano wa kimapenzi na shemegi zao, kuwatii, kuwaheshimu, kuwahurumia na kuwapenda wakwe zake, kuwaandalia chakula kizuri waume zao na kujenga tabia nzuri ya kuvutia kwa jamii na kwa watu wanaohusiana na muume.

Kutokana na umuhimu wa unyago, jamii nyingi za Afrika zimekuwa zikitekeleza utamaduni huu. Moja ya jamii hizo ni ile ya Kiuyu Maambani ambayo inapatikana katika shehia ya Kiuyu Maambani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba. Jamii hiyo imekuwa ikiwaimbia wanawake nyiso pale wanapokuwa katika unyago.

Sababu iliyomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu kwanza ni kwamba katika utalii alioufanya hakuona utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza dhamira na dhima za nyimbo za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani. Pili, mtafiti amevutiwa kufanya utafiti huu kutokana na baadhi ya wanajamii kuziona nyimbo za

nyiso hazina maana na kudai kuwa ni nyimbo zenye kupotosha maadili na kuwaona wale wenye kuimba nyimbo za nyiso kuwa ni watu wasio na ustaarabu. Hivyo utafiti huu uliona ipo nafasi ya kufanyika kwa lengo la kutaka kuzibainisha nyiso na hatimae kuchunguza dhamira na dhima za nyimbo za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Nyimbo ni utanzu wa kale na maarufu sana katika jamii yoyote ulimwenguni. Nyimbo zimekuwa zikifanya kazi ya kusawiri maisha halisi ya jamii ya Waswahili (Waziri, 2016). Watafiti wengi wamewahi kufanya uchunguzi kuhusu nyimbo za jamii mbalimbali baadhi ya watafiti hao ni Khamis (1998), Amer (1998), Moh`d (2015), Ali (2016) na Waziri (2016). Kwa mfano, Ali (2016) alifanya uchunguzi wenye mada "Kuchunguza Dhamira katika Nyimbo za Watoto: Mfano Kutoka Shehia ya Mchangamdogo Kisiwani Pemba." Katika utafiti huo aligundua kwamba nyimbo za watoto za Shehia ya Mchangamdogo zina dhamira ya wizi, utelekezaji wa watoto, umuhimu wa elimu, ukewenza, kukubali wasia na nyenginezo. Naye Moh`d (2015) alichunguza dhima za nyimbo ya ngoma ya msondo wa Pemba. Katika utafiti huo aligundua kuwa nyimbo za ngoma ya msondo zina dhima ya kutoa mafunzo kwa wanandoa kwa kuwafanya wawe wavumilivu, wawe na maelewano baina yao na jamii iliyowazunguka, wawe na maadili mema katika jamii wanayoishi nakadhalika.

Tafiti zilizotangulia zinaonesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani bado hazijafanyiwa utafiti pamoja na ukweli kwamba nyimbo za nyiso katika jamii hiyo ni fani ya fasihi inayotumiwa tangu kale hadi sasa. Aidha, baadhi ya wanajamii wamekuwa na mtazamo kwamba nyimbo hizo ni fani isiyo na faida huku baadhi ya

wanajamii wakiona kwamba nyimbo hizo ni kipengele cha utamaduni wao ambacho kina umuhimu mkubwa. Hivyo basi, tatizo la utafiti huu ni kutaka kuzibainisha nyimbo za nyiso na hatimae kubaini namna nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba zinavyoibua dhamira na dhima.

## 1.4 Lengo la Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza kwa kuzibainisha nyimbo hizo pamoja na kubainisha dhamira na dhima za nyimbo za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani.

### 1.4.2 Madhumuni Mahasusi

Utafiti huu una madhumuni mahasusi yafuatayo:

i. Kubainisha nyiso zinazoimbwa katika Jamii ya Kiuyu Maambani.
ii. Kueleza dhamira zinazojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani.
iii. Kufafanua dhima za nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti yasemayo:

i. Ni zipi nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani?
ii. Ni dhamira zipi zinazojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani?
iii. Ni dhima zipi zinazojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu ni:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yatafaa kuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wataalamu ambao ni walimu, wahadhiri pamoja na maprofesa katika taaluma ya fasihi, wataweza kutumia utafiti huu katika kuandika vitabu na makala ambazo zitachukua nafasi ya kutunza mila na desturi za jamii ya Kiuyu Maambani.

**Kijamii:** Utafiti huu una umuhimu kwa wanajamii wa Kiuyu na jamii nyingine kwani umebainisha namna mila na desturi za jamii ya Kiuyu Maambani zinavyoakisiwa ndani ya nyimbo hizo. Pia, nyimbo hizo zitaingia katika maandishi jambo ambalo limefanya kuwa ni kumbukumbu ya kizazi cha sasa na baadae hasa tukizingatia kuwa hadi leo nyimbo hizo zimebakia kuwa katika masimulizi ya mdomo tu na hazijaingia katika maandishi.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Jamii ya Kiuyu Maambani inazo nyimbo nyingi ambazo zimekuwa zikiimbwa toka kizazi hadi kizazi cha leo. Nyimbo hizo ni kama vile nyiso, nyimbo za watoto, nyimbo za msondo, nyimbo za ngoma ya uganga, nyimbo za kulelea watoto nakadhalia. Kwa sababu nyimbo za jamii hii ni nyingi si rahisi kwa mtafiti kuzitafiti zote kwa wakati mmoja. Hivyo basi, katika utafiti huu, mtafiti ametafiti nyimbo za nyiso za unyago tu ili kuona namna nyimbo hizo zinavyoibua dhima na dhamira mbalimbali katika jamii. Data za utafiti zimekusanywa kwa mbinu ya usaili ambapo mtafiti amekwenda moja kwa moja kuwasaili watafitiwa wanawake mmoja baada ya mmoja ambapo mtafiti ameimbiwa nyimbo za nyiso ambazo baadaye amezitalii na

kuchagua nyimbo zilizotumika katika utafiti huu. Mtafiti amechagua wanawake kwa sababu hilo ndilo kundi mahususi linaloimba ama linaloimbiwa nyimbo za nyiso katika jamii hiyo.

## 1.8 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza imebainisha usuli wa mada ya utafiti, tatizo la uitafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya data hadi utafiti huu kukamilika. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti, katika sura hiyo kuna sehemu kuu tatu ambazo kwanza, ni aina ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani, pili ni dhamira zinazopatikana katika nyimbo za nyiso na tatu ni dhima za nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Sura ya tano ndiyo sura ya mwisho ya utafiti huu ambayo inabainisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURAYA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni utalii wa kina wa machapisho yanayohusu mada inayotafitiwa. Utalii huo hufanywa na mtafiti kwa nia ya kupata uelewa juu ya mada anayoitafiti. Pia, kuona pengo la utafiti linalohitaji kuzibwa. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti amebainisha maandishi ya watafiti kama vile Muhando na Balsidya (1976), Moh`d (2015), Mulokozi (1996), Mungai (2014), Mzee (2016), Waziri (2016), Rashid (2016), Gitonga (2017) na Mohamed (2018) ambao wamewahi kufanya tafiti zao kuhusiana na nyimbo wakiwa na malengo tofauti.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhana

Sehemu hii imefanya ufafanuzi wa dhana muhimu zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Dhana hizo ni maana ya nyimbo, dhana ya jando na unyago, aina za nyimbo, dhamira na dhima za nyimbo.

### 2.2.1 Maana ya Nyimbo

Mulokozi (1996) anasema kwamba wimbo ni kila kinachoimbwa. Maana hii inayotolewa na Mulokozi huweza kuingiza kila utanzu wa fasihi katika wimbo iwapo utaimbwa. Hivyo basi, fasili hii inapingana na ile ya Hamad na wenzake (1972) ambao wameeleza kuwa nyimbo ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Kimuundo nyimbo zinaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi. Nyimbo huweza kuimbwa na kuchezwa kwa kutumia muziki au bila ya kutumia muziki.

Naye Msokile (1981) anafasili nyimbo kwa kusema kuwa ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Anaendela kueleza kwamba wasanii huimba nyimbo baada ya kupata mguso fulani ndani ya jamii. Sanaa ya nyimbo inatofautiana na sanaa ya mazungumzo kwa sababu ya matumizi ya lugha pamoja na vionjo maalumu vya kishairi vinavyoleta mvuto kwa jamii. Mawazo haya yanafanana na yale ya Balisidya (1987) anayeleza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi, zenye kutumia mahadhi ya melodi, mapigo na muwala. Nyimbo huimbwa na watu ambao hujaribu kuelezea uhalisia wa maisha.

Njogu na Chimerah (1999) nao wameeleza kuwa nyimbo zinatokana na ushairi ambao ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe, nyimbo ambazo zilianza na hisia za matukio yaliyowakuta watu katika mazingira yao ya raha na furaha, ugumu wa kujituma ama machungu na ushujaa. Wanafafanua kwamba katika jamii za kilimwengu wimbo ulianza wakati mwanadamu alipobuni lugha, jambo ambalo lilimtoa katika hali ya uhayawani na kumfanya awe kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mwanadamu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango katika kuyakabili na kuyabadilisha mazingira hayo.

Baada ya kutalii fasili hizi za nyimbo katika utafiti huu dhana ya nyimbo imefafanuliwa kama ni utanzu wa fasihi simulizi ambao huweza kughaniwa au kuimbwa, muundo wake huweza kuwa wa mashairi ya kimapokeo ama kimamboleo yaani unaofuata au usiofuata kanuni za urari wa vina na mizani. Nyimbo huweza kuimbwa huku ukichapuzwa kwa kutumia ala za muziki, madoido kama vile upigaji wa kofi, matumizi ya firimbi, mbinja, ngoma, nganja nakadhalika.

### 2.2.2 Jando

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) inafafanua dhana ya jando kama ni chuo kikuu cha watoto wanaume, wanapotahiriwa na kufundishwa mambo ya kiutu uzima. Fasili hii inatufundisha kuwa, jando huwahusu watoto wanaume na wala sio watoto wa kike. Pia, tunapata uelewa kuwa jando hutoa mafunzo mbalimbali kwa watoto ambao hufika jandoni.

Haji na wenzake (1981) wanatubainishia dhana ya jando kwa kusema kuwa kutokana na mila za jamii watu huwa wanatambulishwa rasmi mabadiliko hayo. Ngoma za jadi kama vile jando na unyago zimo katika jamii za Kiafrika ambapo jando kwa kawaida ilikuwa kwa wale wavulana ambao wameshakua wakubwa, kiasi ambacho wanataka waelewe wajibu wao, kuhusu namna ya kuishi katika jamii kwa marika hayo waliyofikia.

Vijana huingizwa jandoni wakiwa na umri kuanzia miaka saba na kuendelea. Wavulana baada ya kutahiriwa wakisubiri kuvuka, walipatiwa mafunzo juu ya maadili bora kuwaheshimu wakubwa, kuwa shupavu, uwajibikaji, jinsi ya kuishi vizuri na mke, namna ya kulinda familia, ukoo na kabila kwa jumla. Yalikuwa mafunzo ya kuwaingiza vijana katika utu uzima.

### 2.2.3 Unyago

Mzee (2016) anafafanua kuwa unyago ni chuo kikuu cha vijana wa kike mahali maalumu, ili kufundishwa maelekezo ya mila na desturi za kabila lao. Tendo hilo kwa kawaida hufanyiwa wasichana ambao wamekwisha vunja ungo. Ni tukio maalumu kwa wasichana fulani waliokwishatoka katika kundi la watoto na sasa wamo katika kundi la watu wazima. Msichana alichezwa unyago kuanzia umri wa

miaka saba na kuendelea, na kwa kawaida msichana akishachezwa unyago huwa tayari kwa maisha ya ndoa. Huko Zanzibar wasichana walifundishwa jinsi ya kutunza nyumba, jinsi ya kutunza watoto, jinsi ya kufanya mapenzi na kujistarehesha na kuwastarehesha waume zao. Katika utafiti huu mtafiti amejikita kuchunguza nyimbo za unyago tu ambazo zinawahusu watoto wakike. Mtafiti hakuchunguza nyimbo za jando ambazo zinawahusu watoto wa kiume.

### 2.2.4 Dhamira

Kwa mujibu wa Ndungo na Wafula (1993) wanafafnua kwamba dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo, dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira katika makundi mawili, nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa mfano, unaweza kuwa na dhamira ya vita vya ukombozi, dhamira ya ujenzi wa jamii, dhamira ya utu bora, uvivu na ulanguzi.

Mawazo ya Ndungo na Wafula yameingia ndani zaidi kuhusu suala la dhamira. Kwa hivyo, yamemsaidia mtafiti namana ya kubaini dhamira katika nyimbo zilizotafitiwa. Hii ni kutokana na kwamba waandishi hao wametoa mifano ya dhamira zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti ameyachukua mawazo hayo na yamekuwa kielelezo katika kutafiti dhamira katika kazi hii.

BAKIZA (2010) wanaeleza kwamba dhamira ni jambo linalozungumzwa na msanii katika kazi ya fasihi. Naye Senkoro (2011) anaeleza kuwa katika dhamira kuu tunaweza kupata dhamira ndogo ndogo zinaoambatana na dhamira kuu. Mawazo haya ya BAKIZA na Senkoro ni kwamba kile kinachoelezwa katika kazi za fasihi

ndicho kinachoelezwa na wahakiki kama ni dhamira katika kazi husika. Aidha, mawazo hayo yanaweza kuwa zaidi ya moja katika kazi ya fasihi.

Vile vile, Madumulla (2009) anaeleza kuwa dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Anaendelea kueleza kuwa Senkoro anatahadharisha kuchanganya dhamira na maudhui, jambo ambalo hutokea kwa wengi. Dhamira ni sehemu tu ya maudhui. Na aghalabu, dhamira kuu ndio hujenga kiini cha kazi ya fasihi. Dhamira kuu ndio husindikizwa na dhamira ndogo ndogo. Wazo kuu hubeba funzo kuu.

Hali kadhalika, Senyamanza (2012) anasema dhana ya dhamira haipaswi kuchanganywa na dhana ya maudhui kwasababu dhana hizo ni tofauti. Dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi yake. Dhamira ni sehemu mojawapo tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Kwa kawaida dhamira kuu ndiyo hujenga kiini cha kazi nzima ya fasihi.

Kwa maoni ya mtafiti ni kwamba, dhamira ni lengo la mwandishi ambalo huazimia kulifikisha kwa jamii ili iweze kujenga au kufuata mwenendo bora wa maisha. Dhamira katika kazi ya fasihi huweza kuwa zaidi ya moja. Kwa mfano, katika riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie* kunapatikana dhamira kama vile umaskini, umuhimu wa elimu, madawa ya kulevya, wizi na ujambazi, ulevi, uongozi mbaya, suala la malezi na kadhalika.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Nyimbo

Katika sehemu hii mtafiti amefafanua maandishi kadhaa ya waandishi watangulizi kuhusu mada inayo tafitiwa. Maandishi hayo yanajikita kwenye aina za nyimbo, dhima za nyimbo na dhamira za nyimbo. Ufafanuzi huo umefanyika kama ifuatavyo:

### 2.3.1 Tafiti Kuhusu Nyimbo

Finnegan (1970) anasema nyimbo zinaweza kutofautiana katika muundo, mtindo, maudhui au dhima, lakini zina kitu kimoja ambacho huzifanya zote zifanane, nacho ni usimulizi. Kutokana na tofauti hizo Finnegan ameziweka nyimbo katika makundi mbalimbali. Miongoni mwao ni nyimbo za kisiasa, nyimbo za watoto, nyimbo za kazi, kama vile kilimo, uvuvi, ukwezi, ulinzi na uwindaji. Nyimbo hizo zinaelezea mambo yanayojitokeza katika jamii kama vile kufunza, kuelimisha, kuburudisha na kuliwaza.

Naye Mulokozi (1996) amegusia aina za nyimbo za Kiafrika, na kuziweka katika makundi kama vile nyimbo za kidini, nyimbo za kazi, nyimbo za vita, nyimbo za taifa, nyimbo za kuwindia, nyimbo za watoto, nyimbo za jando na unyago na nyimbo za harusi. Nyimbo zote hizo, zinasimulia na kuelezea mambo yanayotokea katika jamii zikiwa na lengo la kufunza, kuelimisha na kukosoa.

TAKILUKI (1981) wamezungumzia kuhusu mbolezi ambazo ni nyimbo za kuomboleza. Wanafafanua kuwa jamii nyingi za Kiafrika huzitumia nyimbo hizo wakati wa msiba, wakati mwingine huwa kasida na huimbwa katika nyakati tofauti. Kwa mfano, hapa Zanzibar nyimbo hizi huimbwa wakati wa kupamba maiti, kubeba jeneza na kuelekea makaburini, baada ya mazishi na wakati wa kumkumbuka marehemu. Katika Afrika, nyimbo hizi huimbwa katika nchi ya Nigeria na Ghana. Ingawa TAKILUKI wanaona kuwa Nigeria na Ghana ndio nchi pekee zinazoimba mbolezi lakini ukweli ni kwamba nyimbo hizo hupatikana kila pembe ya Afrika ikiwemo Tanzania. Kwa mfano, wakati wa misiba ya kitaifa hapa Tanzani, tumekuwa

tukishuhudia mbolezi zikiimbwa katika vyombo vya habari na kwenye mikusanyiko ya tanzia hizo.

Mtaalamu mwengine aliyezungumzia utanzu wa nyimbo ni Mbarouk (1983) ambaye ameandika kitabu cha nyimbo za michezo ya watoto. Katika kitabu hiki Mbarouk anasema, kila jamii ya watu huwa na michezo yao ya jadi ambayo huchezwa na watoto wa jamii ile. Michezo hii mara nyingi huambatana na nyimbo. Katika kisiwa cha Pemba kwa mfano, iko michezo mingi ya watoto ambayo hutofautiana kutoka sehemu moja na nyengine, jambo ambalo ni muhimu katika michezo hii ni nyimbo ambazo ndizo zinazochukuwa nafasi ya uzuri wa michezo hiyo.

Kimsingi mtafiti baada ya kutalii aina hizi za nyimbo kama zilivyojadiliwa na waandishi waliotajwa hapo juu imebainika kwamba kuna misingi miwili mikuu ambayo hutumiwa na wataalamu wa fasihi katika kuzibainisha nyimbo. Misingi hiyo wa kwanza, ni ule wa kuangalia dhima ama dhamira zinazojitokeza katika nyimbo husika kama tulivyoona maelezo ya Finnegan (1970), TAKILUKI (1983) na Mulokozi (1996) hapo juu. Msingi wa pili huegemea hadhira ya nyimbo hizo. Kwa msingi huu tunapata nyimbo kama vile nyimbo za watoto kama zinavyoelezwa na Mbarouk (1983) hapo juu. Hivyo utafiti huu umetumia msingi wa dhima katika kuzibainisha nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani.

### 2.3.2 Tafiti Kuhusu Dhima za Nyimbo

Waziri (2016) anamnukuu Lucas (1975) ambaye amaezungumzia kuhusu nyimbo za msanja na jando ambazo ni katika utamaduni wa mwafrika, mfano Zanzibar. Nyimbo hizi huimbwa sana katika maeneo ya Kusini mwa visiwa hivi ambazo hulenga kutoa mafunzo, malezi na maadili mema yanayowasaidia wanajamii kujua namna ya kuishi

kulingana na matumizi ya nyimbo hizi. Naye Nkwera (1978) kwa upande wake anafafanua nyimbo kuwa ni kipengele muhimu cha ushairi ambacho hubeba mafundisho ya hekima na malezi ya busara. Maelezo haya yanatupatia uelewa kwamba nyimbo zina umuhimu mkubwa kwa jamii.

Aidha, Msokile (1981) anafafanua dhima za nyimbo kuwa ni lazima zilingane na hadithi, zikubaliane na jamii katika kupokea ujumbe. Gibbe (1980) nae kwa upande wake anafafanua kuwa nyimbo hutumika kuwaelimisha wanandoa kuwa na maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, hekima na kuwa na adabu nzuri. Ameir (1998) amegundua kuwa nyimbo za watoto zina tafsri kubwa kiutamaduni, kimaisha na kimalezi. Tunakubaliana na mawazo haya yanayotolewa na Msokile, Gibe na Amer kuhusu dhima za nyimbo katika jamii. Kutokana na umuhimu huu kwa jamii ndio maana jamii za Afrika na nyimbo ni kama pande mbili za sarafu moja ambazo haziwezi kutenganishwa.

Nyimbo zinatumika sana kuhakikisha kuwa elimu inawaingia mabinti hao. Pia miiko ya jamii ilielekezwa kwa njia ya nyimbo. Kwa ujumla unyagoni binti hufunzwa mambo mengi sana ya maisha na kwa yule aliyeweza kuyashika kikamilifu na kuyatumia basi alionekana kuwa ni binti mwenye heshima kubwa na aghlabu alipata mchumba wa kumuoa mapema sana katika jamii hiyo. Waziri (2016) anamnukuu Seif (2011) akieleza kuwa unyago humuandaa mwanamke (msichana) kukabiliana na utu uzima, hii ni pamoja na ndoa, miiko ya mila na mafunzo ya maisha kwa ujumla. Unyago ni chuo muhimu sana kwa jamii. Huko unyagoni binti walielekezwa kujitunza na kuwa waangalifu ili kuepuka kupata uja uzito bila ya mpangilio kabla ya kuolewa.

Rashid (2013) alifanya utafiti wenye mada ya utafiti "*Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi."* Utafiti huo uligundua kuwa jamii ya Wahiyao wanatumia jando na unyago kama sehemu ya kuonesha utajiri na ufukara wao. Vijana wanaowekwa jandoni na unyagoni ni wa umri mdogo kati ya miaka 2-5. Rashidi anasema kwamba kwasababu ya umri wao mdogo hawawezi kutunza mafunzo ya jando na unyago. Athari yake ni kwamba watoto hao hukosa mafunzo imara na hatimae ni kujiingiza katika uvunjifu wa maadili ikiwemo kushiriki katika uasharati na hivyo kupata mimba za nje ya ndoa.

Utafiti wa Rashidi ingawa ulijikita katika jamii tofauti hata hivyo umetupa uelewa kwamba nyiso zina dhima ya kuwaandaa vijana kuwa salama katika maisha yao kama vile kupiga vita uasharati jambo ambalo linaweza kuhatarisha maisha yao katika wakati huu wa gonjwa hatari la UKIMWI. Hivyo basi, utafiti huu umeyachunguza mawazo haya na kuona iwapo yanajitokeza au la katika nyiso zilizotafitiwa.

Vile vile, Mungai (2014) alifanya utafiti wenye mada *"Fani katika Nyimbo za Anastacia Mukabwa."* Mwimbaji huyu ni wa nchini Kenya. Katika utafiti huo anaeleza kuwa nyimbo ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ambazo zina mwelekeo wa matumizi ya lugha yenye sauti zenye mahadhi na midundo iliyotengwa ili kunasa hisia za hadhira**.** Nyimbo hunasibika kwa mpangilio maalum wa maneno, vipashio vya kiisimu, mada za kimaudhui, kupitia midundo maalum na ujenzi wa taswira. Nyimbo huwakilisha mawazo, fikra na falsafa ya mtunzi kwa njia inayosababisha changamoto na mawasiliano kwa hadhira lengwa. Kwa hivyo, tuna ushahidi wa kutosha kwamba nyimbo za Kiswahili zina ukwasi mkubwa wa

vipengele vya kifani na maudhui vinavyopaswa kuchunguzwa katika kiwango cha usomi. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba nyimbo za Anastacia Mukabwa zina ukwasi mkubwa wa fani na maudhui kama vile wahusika, maudhui, mandhari, toni, tamathali za semi, sitiari, ishara, umbo na mtindo.

Utafiti huu ingawa ulikuwa na malengo tofauti na yale ya utafiti unaotarajiwa kufanyika lakini ulikuwa ni muhimu sana katika kusukuma mbele hadi kukamilika kwa malengo ya utafiti huu. Kwanza, mtafiti alipata maana ya ndani iliyojadiliwa na Mungai kuhusu dhana ya nyimbo. Mjadala huo ulimpatia uelewa mtafiti kwamba nyimbo haziko kwa ajili ya kuburudisha tu bali ni utanzu ambao huwa na dhima mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuonesha falsafa ya jamii.

Utafiti mwengine ni ule wa Moh`d (2015) ambaye alichunguza dhima za nyimbo ya msondo wa jamii ya Wapemba. Katika utafiti huo aligundua kuwa nyimbo za msondo katika jamii ya Wapemba zina dhima ya kuelimisha, kuburudisha, kuwafunza wanandoa na kadhalika. Ingawa utafiti huo ulijikita kutafiti nyimbo za ngoma ya msondo lakini mtafiti alifaidika na utafiti huo kutokana na kuona namna dhima zinavyoweza kutafitiwa katika nyimbo. Tofauti ni kwamba utafiti wa Moh`d ulijikita kwenye nyimbo za msondo lakini utafiti huu umejikita kuchunguza nyiso.

Naye Mzee (2016) alifanya utafiti uliohusu kuchunguza nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini Unguja. Katika utafiti huo anaeleza kuwa wapo wanajamii wanaoamini kwamba nyimbo hizo za singo zimekua zikikiuka maadili na zimekuwa zikitumiwa na watu wasiokuwa na ustaarabu. Hata hivyo utafiti wa Mzee ulionesha kuwa nyimbo za singo hufundisha mwanamwari taaluma inayofaa ya kukabiliana na maisha yake ya ndoa, kuwatimizia waume haki zao, kujenga moyo wa subira katika

kukabiliana na matatizo, kuishi vizuri na majirani, kuepuka uhusiano wa kimapenzi na shemegi zao, kuwatii, kuwaheshimu, kuwahurumia na kuwapenda wake zake, kuwaandalia chakula kizuri waume zao na kujenga tabia nzuri ya kuvutia kwa jamii na kwa watu wanaohusiana na muume.

Utafiti wa Mzee (ameshatajwa) una umuhimu mkubwa katika kufikia lengo la utafiti huu. Utafiti huu umemsaidia mtafiti katika vipengele kadhaa. Kwanza, Waziri alichunguza dhima za nyimbo za singo kama ilivyofanyika katika utafiti huu. Pia, ametuonesha namna nyimbo zinavyoweza kutafitiwa kwa misingi ya fasihi simulizi. Tofauti ya utafiti wake na utafiti huu ni kwamba yeye alijikita kuchunguza nyimbo za singo za jamii ya Uzini Unguja lakini utafiti huu umejikita kuchunguza nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani kisiwani Pemba.

Vile vile Gitonga (2017) alifanya utafiti wa nyimbo akiwa na mada *"Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili."* Katika utafti huu aligundua kuwa kuna baadhi ya dhima na dhamira zimelingana katika harusi za Kimeru na zile zilizotafitiwa. Ingawa utafiti wa Gitonga haukuhusu nyimbo za nyiso moja kwa moja, utafiti huo umekuwa na manufaa katika kufikia lengo la utafiti huu kutokana na kwamba baadhi ya nyimbo za harusi za Kimeru zina aina fulani ya kufanana dhamira na dhima na nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Kwa sababu hiyo kwanza, mtafiti amejifunza namna ya kukusanya, kuwasilisha na hatimae kuchambua data za utafiti zihusuzo nyiso. Pili, mtafiti amepata uelewa wa kina wa namna utafiti unaohusu dhamira na dhima unavyoweza kufanyika hatua kwa hatua. Kwa miktadha hiyo mtafiti ameyatumia mawazo ya Gitonga na hatimae

kukamilisha utafiti wake unaohusu dhima za za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani.

Aidha, Mohamed (2018) alifanya utafiti wenye mada *"Usasa wa Mashairi ya Nyimbo za Taarab ya Sasa: Fani na Maudhui."* Katika utafiti huo aligundua kuwa kuna mitazamo changamano kuhusu mashairi ya taarab ya kisasa. Wapo wanajamii wanaoamini kwamba mashairi hayo yanafaa na wapo wanaoamini kwamba hayafai kwani yanalenga utusi, upasho pamoja na unyanyapaaji wa namna kwa namna.

Kama ilivyokuwa kwa tafiti nyengine zilizojadiliwa hapo juu, utafiti wa Mohamed (2018) nao haukugusia nyimbo za nyiso. Hata hivyo mtafiti amefaidika na utafiti huo na kutoa mchango wa kufikia lengo la utafiti huu kutokana na kujadili vipengele vya maudhui, dhamira vikiwemo kama utafiti huu ulivyojikita katika lengo la pili la utafiti huu. Pia, katika utafiti huo kuna mjadala wa mawazo yanayohusu mitazamo changamano kuhusu mashairi ya taarab ya kisasa kama ilivyo kwa utafiti wetu ambao nao umechipukia kutokana na mitagusano na mivutano kuhusu dhima za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani kwani wapo wanaoona kuwa kwa sasa hazina mchango wowote wa kuimarisha jamii na wapo wanajamii wanaoamini kwamba nyiso ni chuo endelevu cha kuwafunza wasichana kuyakabili maisha.

## 2.4 Pengo la Utafiti

Mtafiti ametalii machapisho kadhaa yanayohusu mada iliyotafitiwa. Machapisho hayo yamejikita kufanya uchunguzi wa vipengele mbalimbali vya fani na maudhui kama sehemu ya fasihi. Hata hivyo hakuona kazi iliyowahi kufanyika ikiwa na lengo la kuchunguza dhima za nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani katika kisiwa cha Pemba. Hivyo basi, mtafiti aliona ipo haja ya kufanya utafiti huu kwa vile jamii

hiyo imekuwa ikitumia nyiso huku baadhi ya wanajamii wakiona kwamba hazina dhima zozote. Kwa mantiki hiyo mtafiti alitaka kulithibistisha swali hili kwa misingi ya kisayansi.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Sengo (2009) anaifasili dhana ya nadharia kuwa ni muongozo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsusi kwa kutoa maoni, mwelekeo au falsafa juu ya matumizi ya taratibu za utafiti. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Nadharia hii imefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### 2.5.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inajadiliwa na Wamitila (2002) kuwa ni nadharia inayorejelea mitizamo au tabia fulani za usomaji wa matini zinazohusisha uhakiki wa aina mbalimbali ambayo huangaza dhima na majukumu ya msomaji katika matini au kazi za fasihi.Waasisi na watetezi wa nadharia hii ni Fish (1980), Tompkins (1980),Wolfgang (1974), Barthens na wengine.

Lengo la kimsingi la nadharia hii ni kuwabainisha wasomaji, kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji.Wahakiki wanaojishughulisha na nadharia hii wanaelekea kuwa na mtazamo tofauti na ule wa kijadi wa kuiangalia fasihi kama kitu kilichokamilika. Hawa wanaamini kuwa, maana yeyote ya kifasihi inategemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Msomaji husawiriwa kama mwenye mchango mkubwa katika kubuni maana ya kazi husika ya fasihi. Hii ni sawa na kusema kuwa si rahisi kudai kuwa kuna maana fulani sawa na sahihi zaidi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji.

Wasomaji wanaweza kuvifasiri vipengele vya kiisimu na kisanaa kwa namna mbalimbali.Tofauti hizo za maana huweza kusababishwa na vipengele mbalimbali vya kimsingi vinavyounda mwitiko wa msomaji. Tofauti kati ya ubaki wa matini husika na hisia za kibinafsi za msomaji anayehusika na utofauti wa namna matini inavyoelekeza au kutatiza. Sifa hiyo ni ile inayowezesha kuwepo kwa maana au fasili mbalimbali za kazi moja ya fasihi.  Kimsingi mtafiti anakubaliana na mawazo ya nadharia hii kwani yanampa msomaji uhuru wa kuweza kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kwa kadri ya uelewa na tajriba ya msomaji husika kuhusu masuali mbalimbali ya kijamii. Kwa mujibu wa Wafula (2007) waitifaki wa nadharia hii huuliza maswali ambayo kwayo huibua misingi ya nadharia hii. Maswali yanayoulizwa ni:-

a) Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?
b) Je, kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia?
c) Kuna wasomaji ambao husoma na kutafsiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine?
d) Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Adena (1971) anadai kuwa kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kwamba:

(1) Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela.

(2) Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi.

Wasomi mbalimbali hufasiri athari hizo kupitiaa njia tofauti tofauti kutegemea:

(i) Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.

(ii) Namna matini inavyoelezea au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa inayozua usomaji mzuri au mbaya wa kazi inayohusika.

(3) Wananadharia hawa wanashikilia kuwa kuna njia mbili za kusoma kazi ya fasihi ambazo ni:-

(i) Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejulikana na kutambuliwa na msomaji.

(ii) Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kuchochea msomaji kujitafutia nakujiamulia.

Ujumbe uliomo katika kazi anayoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa mara kadhaa ili msomaji aelewe matini anayosoma.

(4) Usomaji ni tendo linalofanyika na kutekelezwa kwa wakati maalum, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri sana maana ya matini hiyo. Fish anadai kwamba wasomaji wanapaswa kufanya mikabala ya aina fulani na Matini hizi katika mikitadha mbalimbali.

(5) Msomaji anayetumia mkakati wa mwitiko kusoma kazi ya sanaa hufuata hatua tatu katika weledi wa kazi ya fasihi.

(i) Hurejelea kazi inayosomwa kwa kutafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.

(ii) Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji.

(iii) Hudhihirisha kwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.

(6) Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

Nadharia hii inaonekana kuwa inaweza kufikisha lengo la utafiti huu; Sababu kubwa ni kwamba lengo la utafiti huu ni kuchunguza na kubainisha nyiso, dhamira na dhima za jamii ya Kiuyu Maambani. Kwa hiyo, pamoja na baadhi ya wahakiki kama vile Wamitila (2002) kueleza kuwa nadharia hii inakosolewa kutokana na kuifanya kazi ya fasihi kutokuwa na maana hadi pale itakapopewa maana na msomaji, mtafiti ameona kuwa nadharia hii imekuwa na faida katika kufikia malengo ya utafiti huu. Hivyo mtafiti aliona kuwa hakuna mapungufu yanayoweza kujitokeza kutokana na kuitumia nadharia hii.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameelezea kazi tangulizi alizozitalii zinazohusiana na mada iliyotafitiwa. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza imewasilisha dhana mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Sehemu ya pili imewasilisha maandishi yaliyowahi kuandikwa pamoja na kutafiti nyimbo za aina mbalimbali. Kufanya hivyo kumemuwezesha mtafiti kubainisha pengo la utafiti huu.

Aidha, katika sura hii mtafiti amefanaya ufanuzi wa nadharia ya Sosholojia na Mwitiko wa Msoamaji ambazo zimeongoza utafiti huu.

# SURA YA TATU

# BINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafanya ufafanuzi wa vipengele vya mbinu za utafiti zilizotumiwa na mtafiti hadi utafiti huu kukamilika. Kwa hivyo sura hii imewasilisha umbo la utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, data na mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchambuzi wa data na hitimisho.

## 3.2 Umbo la Utafiti

Usanifu wa utafiti ni dira ambayo inaelekeza utafiti utakaofanywa utakuwa ni wa aina gani na utahusisha mbinu za aina gani (Robson, 2007). Utafiti huu umetumia umbo la kimaelezo. Kothari (2008) anaeleza kuwa umbo la kimaelezo katika utafiti ni pale data zinapokusanywa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Anaendelea kueleza kuwa utafiti unaotumia umbo la kimaelezo, data huwa haziwasilishwi kwa kutumia tarakimu. Pia, umbo la kitarakimu huwa ni pale data zinapofanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kwa njia ya tarakimu. Hivyo, data za utafiti huu zimekusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo hii ni kwa sababu utafiti huu unajikita kwenye sanaa ya lugha.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ni utafiti wa uwandani. Hivyo basi, umefanyika kenye nyiso zilizokusanywa katika kijiji cha Kiuyu Maambani, Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba. Sababu ya kuchagua eneo hilo ni kwamba mtafiti aliamini atapata data zitazojibu maswali ya utafiti huu. Pia, eneo hili ni muhimu kwani nyiso za kijiji

cha Kiuyu Maambani ni miongoni mwa tanzu za fasihi ambazo hazijawahi kutafitiwa katika kipengele cha dhima.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2008) walengwa wa utafiti ni jumla ya watu, wanyama au vitu ambavyo vimekusudiwa kufanyiwa utafiti. Kundi lengwa ndilo ambalo hujumuishwa katika matokeo ya utafiti. Kwa hivyo, walengwa wa utafiti huu ni nyiso za jamii ya watu wa Kiuyu Maambani, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mtafiti amechagua jamii hii kwa sababu ni jamii ambayo hadi leo inatekeleza unyago ambao huambatana na nyimbo za nyiso. Hivyo, ilionekana ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kuweka wazi dhima ya nyimbo za nyiso katika jamii hiyo kwa misingi ya kisayansi.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Enon (1998) anaeleza kuwa usampulishaji ni kitendo cha kuchagua kikundi kidogo cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa. Katika utafiti kundi hili dogo huchaguliwa na mtafiti ili kutoa data na hatimae kuliwakilisha kundi kubwa linalotafitiwa. Hili hufanyika kwa sababu sio rahisi kutafiti kundi lengwa zima. Zipo mbinu kadhaa ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini utafiti huu umetumia mbinu ya uteuzi wa sampuli ya lengo maalumu. Sampuli ya malengo maalumu hulenga kuchagua sampuli ambayo mtafiti anaamini kuwa itajibu maswali ya utafiti anaoufanya.

#### 3.5.1 Sampuli

Sampuli ni sehemu ya watafitiwa ambao huteuliwa ili kuwa wawakilishi ambao hufanywa kuwa kundi lengwa la utafiti (Kombo na Tromp, 2006). Sampuli ya utafiti

huu ilikuwa ni nyiso zilizokusanywa kutoka kwa wanajamii wa Kiuyu Maambani ambao wanazitambua nyimbo za nyiso. Jumla ya sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni nyimbo 17, ambazo zimeimbwa na wanawake wenye umri kati ya miaka 45-68 ambao waliwahi kuhudhuria kwenye shughuli za unyago na wanazielewa nyiso za jamii iliyotafitiwa. Idadi ya wanawake hao walikuwa 11. Utafiti huu umeteua wanawake bila kuwemo wanaume kwani nyiso za jamii hiyo huimbwa na wanawake tu. Wakati wa kuwafanyia usaili, mtafiti alirekodi sauti za nyimbo zilizoimbwa kutoka kwa msailiwa mmoja mmoja. Vile vile, alirikodi katika shajara baadae alizifanyia uchambuzi na kupata nyimbo 17 kati ya 30 zilizokusanywa. Na baada ya kuziteua nyimbo hizo mtafiti amezifanyia uchambuzi ili kuzibainisha aina za nyimbo hizo, kubainisha dhamira na dhima zinazopatikana katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani

### 3.5.2 Usampulishaji

Uteuzi wa sampuli tajwa hufanyika kwa mtafitiwa kutaja mtu mwengine ambaye pia anaweza kutoa taarifa zinazohusiana na utafiti unaofanyika. Powell na Conway (2004) wanasema kuwa mtafiti anapotumia mbinu ya sampuli tajwa huwafuata watafitiwa ambapo huwapata kibahati nasibu. Baada ya kukusanya data kwa mtu mmoja humpa nafasi ya kutaja mtu mwengine anayemjua na ambaye atasaidia katika kutoa data.

Hivyo basi, mbinu ya usampulishaji tajwa imetumika kukusanya data za utafiti huu kutoka kwa watafitiwa wanawake ambao walitajwa kwamba wana uelewa kuhusu nyimbo za nyiso. Hii ni kwa sababu katika jamii ya Kiuyu Maambani waimbaji wa nyimbo za nyiso ni wanawake tu. Kwa kawaida wanaume hawaimbi nyiso kwani

huambatana na matendo ambayo hayapaswi kuyajua wanaume. Mtafiti amechagua njia hii kwa sababu aliamini kwamba kwa kutumia njia hii angepata data za utafiti huu kwa urahisi.

### 3.6 Data za Utafiti

Katika utafiti wowote wa kisayansi mtafiti hukusanya data za msingi na data za upili. Katika utafiti huu mtafiti amekusanya data za msingi na za upili ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Hivyo upatikanaji wa data za msingi na data za upili katika utafiti huu umefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

#### 3.6.1 Data za Msingi

Salim (2015) anamnukuu Furlong (2000) akieleza kwamba data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti. Kwa kawaida data hizo huwa hazijakusanywa kama sehemu ya utafiti mwengine wowote. Young (1984) ansema kwamba data za msingi zinapofanyiwa uchambuzi na kuandikwa kama sehemu ya tasnifu hugeuka na kuwa data za upili. Data za msingi ambazo ni nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zimekusanywa kwenye nyimbo hizo baada ya kukusanywa kutoka kwa wanajamii wa Kiuyu Maambani ambao wanauelewa kuhusu nyimbo za nyiso.

#### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbali mbali (Creswell, 2009). Salim (2015) anaeleza kuwa data za upili hutumiwa na mtafiti katika kuandika pendekezo la utafiti na ndizo humpatia mtafiti pengo la utafiti wake. Vile vile, data za upili hutumika katika kushadidia data za msingi wakati wa

kuandika sura ya nne ambayo inahusu uwasilishaji wa data za utafiti. Hivyo data za upili za utafiti huu zimepatikana kutokana na mtafiti kutalii majarida, tasnifu, wavuti na tovuti na vitabu.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (2008) anaeleza kuwa mbinu ya ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti. Utafiti huu umekusanya data zake kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka na mbinu ya usaili. Mbinu ya usaili imetumika kukusanya data za msingi na mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilitumika kukusanya data za upili. Mtafiti amezipata nyimbo hizo kwa kuimbiwa na wanawake ambao wanazitambua nyimbo za nyiso ambapo waliziimba huku mtafiti akizirekodi katika shajara. Baadaye mtafiti alizitalii nyimbo hizo na kuchagua nyimbo 17 kati ya nyimbo 30 ambazo aliamini zitajibu maswali ya utafiti huu.

#### 3.7.1 Mbinu ya Usaili

Kothari (2013) anasema kuwa usaili ni majibizano ya ana kwa ana au kwa simu kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Katika utafiti huu mtafiti amekusanya data za msingi kwa kufanya usaili na sampuli ya watafitiwa. Mtafiti aliona kuwa njia hii ni bora kwa sababu baadhi ya watafitiwa walikuwa hawajui kusoma na kuandika hivyo ni vigumu kutumia mbinu ya hojaji. Pia, mtafiti anaiona mbinu hii imekuwa bora kutokana na ukweli kwamba imetoa fursa ya kutoa maelezo kwa watafitiwa kuhusu mada ya utafiti huu. Data za msingi ambazo ni nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ndizo zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili moja kwa moja kwa watafitiwa.

Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti ameandaa daftari maalumu ambalo ameligawanya katika sehemu kuu tatu na kila sehemu ikiwa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengo mahususi ya utafiti huu. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data. Mtafiti amewafuata wanawake mmoja mmoja na wamemuimbia nyimbo za nyiso mmoja mmoja huku wakitoa maelezo kuhusu dhima na dhamira zinazopatikana katika nyimbo hizo.

### 3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka

Neno "nyaraka" kama lilivyotumika katika utafiti huu ni machapisho na maandiko yanayopatikana katika maktaba. Mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kudurusu machapisho yanayohusiana na mada inayotafitiwa (Kothari, 2004). Data za upili pamoja na kutumika katika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi katika uchambuzi wa data pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasnifu inayohusika na "mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia." Data za upili katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na maktaba kuu Zanzibar. Maeneo mengine yaliyotumika ni maktaba ya Chuo Kikuu cha Chukwani pamoja na kutalii mitandao ya intaneti na hatimae kupata maarifa mapya kutokana na kazi zinazohusu madaya iliyotafitiwa.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013) ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti huu mbinu ya uchambuzi wa data iliyotumika ni

mbinu ya mkabala wa kimaelezo. Mtafiti alichambua data ambapo alianza kuzibainisha aina za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani, kisha ameelezea dhamira zinazopatikana katika nyiso hizo na mwisho amefafanua dhima za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii inahusu mbinu za utafiti. Katika sehemu hii mtafiti amebainisha mbinu za utafiti ambazo amezitumia hadi utafiti huu ulipokamilika. Imeelezwa kuwa data za msingi za utafiti huu zimekusanywa kwenye nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ambapo jumla ya wanawake 11 waliowahi kuhudhuria katika shughuli ya unyago na wanazielewa nyiso za jamii hiyo walishiriki kutoa data za utafiti huu. Pia, data za upili zimekusanywa kutoka katika machapisho mbalimbali ya waandishi na watafiti waliotangulia.

# SURA YA NNE

## UWASILISHAJI NA UCHAMBUZIWA DATA ZA UTAFITI

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti kwania ya kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti. Uchambuzi huu wa data umegawanywa katika sehemu tatu kuu ambazo ni kubainisha nyiso, kueleza dhamira za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani na kufafanua dhamira za nyiso za jamii hiyo. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya Sosholojia na Mwitiko wa Msomaji.

### 4.1 Nyimbo za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni zipi nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani? Mtafiti baada ya kuzikusanya data na kuzichambua aligundua kuwa nyimbo hizo zinaweza kuwekwa katika makundi yafuatayo kutegemea dhima zinazojitokeza katika nyimbo hizo.

#### 4.1.1 Nyimbo Zinazofunza Usafi

Kutokana na uchambuzi alioufanya baada ya kuzikusanya data zake, mtafiti amebaini kuwa aina ya kwanza ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ni zile ambazo zinahimiza usafi miongoni mwa wanawake. Mfano wa wimbo unaohimiza usafi ni wimbo namba nne (4), wimbo wa *Mwari*. Wimbo huo unaeleza:

Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua
Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua

Wimbo huu hutumiwa na jamii ili kuonesha umuhimu wa mwanamke kutunza usafi wa mwili wake kwa kuoga. Kuchanja mvua kwa maana iliyokusudiwa hapa ni kuoga kwa kutumia maji ya mvua wakati mvua inanyesha. Aidha kwa njia ya kujimwagia mwenyewe au kutoka kwenye mchirizi wa mvua au bomba refu lililosimama. Hii ni ishara ya kujisafisha na kutunza usafi wa mwili, jambo ambalo ni muhimu sana hasa kwa mwanamke katika jamii ya Waswahili. Wimbo mwengine ambao unaingia katika aina hii ya nyimbo ni wimbo namba sita (6), wimbo wa *Ruwanja*. Wimbo huo unaeleza hivi:

> Mfywagirire mfyagirire ruwanja
> Mwenzenu wangweta hao wakifyagira
> Mfwagirire aee mfyagirire ruwanja

Kupitia wimbo huo, watoto wakike wanafundishwa kutunza usafi wa mwili pamoja mazingira. Wakati wa kuimba wimbo huu mtafitiwa alimueleza mtafiti wa kazi hii kwamba pamoja na mambo mengine yanayohimizwa kuhusu usafi ndani ya wimbo huu, watoto wa kike wanatakiwa wasafishe sehemu za siri pale watapokuwa katika ndoa. Hii inasisitiza umuhimu wa wanawake kuwa wasafi kama sehemu ya utamaduni ambao unalenga kumfanya mwanamke huyo awe ni mwenye mvuto wa mapenzi pale atapokuwa katika ndoa.

Jamii ya Waswahili wa Pemba wanapenda sana utamaduni wa kuhifadhi usafi wa sehemu zao za siri, hasa pale wanapokuwa katika ndoa. Kuweka uchafu katika sehemu za siri kwa mwanamke katika utamaduni wa Pemba ni uchuro na jambo lisilokubalika katika jamii ya watu hawa. Uzoefu wa mtafiti uliuoongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji unaompa fursa ya kuhakiki mambo kwa uzoefu alionao.

### 4.1.2 Nyimbo zinazokuza Umoja na Mshikamano

Data zinaonesha kuwa baadhi ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaweza kubainishwa katika kundi la nyimbo ambazo zinalenga kujenga umoja na mshikamano katika jamii. Kwa mfano, wimbo namba tisa (9), wimbo wa *Kumekucha* unaingia katika kategoria hii. Wimbo huo unaeleza hivi:

> Kumekucha eee
> Kumekucha kumenanauka
> Mwenye tama na atamauke
> tupe mamae harusi
> Tupe kinura mgongo

Watafitiwa walioimba wimbo huu walieleza kuwa wimbo huo umekuwa ukiimbwa na wanawake majirani wa mama wa mtoto wa kike akiwemo somo wa mtoto wa kike huyo wakati wa asubuhi ya kuamkia siku ya harusi. Hii ni baada ya mkesha wa usiku mzima ambapo wanawake hao walikuwa wakimfundisha mtoto wa kike namna ya kuishi katika ndoa yake. Kutokana na hali hiyo wanawake hao hujenga umoja na mshikamano na mama hufarijika. Wimbo huo huimbwa katika miktadha hiyo kwani nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani hazimalizii kwenye tukio la unyago tu na badala yake ni zoezi endelevu la kutoa mafunzo hayo.

### 4.1.3 Nyimbo Zenye Kuonya

Jamii ya leo imejaa tamaa ya watu kutaka kufanya ngono holela kama hali hiyo inavyosawiriwa katika Medical Aid Foundation katika tamthiliya ya *Kilio Chetu* (2004). Hivyo wimbi la vijana hao limekuwa likiwashawishi wengine kufanya ngono holela. Kutokana na hali hiyo, katika jamii ya Kiuyu Maambani zipo nyimbo za nyiso ambazo zimekuwa zikiwaonya wasichana kutofanya hivyo. Kwa mfano, wimbo namba tano (5), wimbo wa *Kiazi*. Wimbo huo unaonya hivi:

Kiazi mama kiazi cha nyelele
Kiazi simpi somo kiazi kinyelele
Kina mafundo mafundo, juu kinaota nywele

Katika wimbo huu watoto wa kike wanaonywa kutoshiriki katika ngono kwa kutumia mbinu ya tafsida “kiazi simpe somo, kiazi kinyelele” ambapo wanawake wanaonywa kuwa hata watu wao wa karibu kamwe wasikubali kufanya nao ngono. Kwa ujumla hili ni onyo wanalopewa wanawake wa jamii hiyo kwani kufanya ngono holela kunapoteza hadhi ya mwanamke katika jamii hiyo. Wimbo mwengine wenye kuingia katika kundi la nyimbo zinazoonya ni wimbo namba saba (7), wimbo wa *Kigugusi*. Wimbo huo unasimulia hivi:

Kigugusi amwambia unyayo
Ukatazwalo ndilo ufanyalo
Mgeni wetu wajana na leo kaja

Wimbo huu unawaonya watoto wa kike wasiwe na tabia ya kujipeleka mbele ya wageni wanapokuja. Mtafitiwa alieleza kuwa, onyo hasa linalohimizwa hapa ni kwa watoto wa kike ambao ni makamo kujipeleka mbele ya wanaume wageni. Hii inatupatia picha ya namna jamii ya iliyotafitiwa na Afrika kwa ujumla inavyowalea watoto wa kike kutojishirikisha na wanaume ambao huweza wakakawataka kimapenzi kwani mwanamke ambaye anafanya mapenzi kabla ya ndoa yake anaonekana kuwa hana thamani yoyote pale atapoingia katika uhusiano wa ndoa.

### 4.1.4 Nyimbo za Kuhamasisha Kazi

Aina nyengine za nyimbo za nyiso zinazopatikana katika jamii ya Kiuyu Maambani ni zile zinazohimiza kazi. Mfano wa nyimbo hiyo ni wimbo namba kumi na moja (11), wimbo wa Mzimu ambao unaeleza hivi:

Sona sona sona mzimu sona
Mzimu huu wa nani
Mzimu huu wa tate
Watate wali perere
Waliperere watinya
Tulisake sake
Tulisaure saure
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande

Wimbo huu huimbiwa watoto ili kuonesha umuhimu wa kufanya kazi hasa kushiriki katika kilimo. Katika wimbo huu mwimbaji anaposema "Nyikanga hao tuwape mbeu wapande" inalenga kuwafundisha kuwa nao wanaweza kushiriki katika uzalishaji mali kama vile wanavyofanya wanaume katika jamii hiyo. Kutokana na haya, wanawake hao hujikuta wakishiriki katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa jamii mpaya kama vile kilimo.

### 4.1.5 Nyimbo Zinazofunza Maisha ya Ndoa

Data zinaonesha kuwa zipo nyimbo ambazo zinalengo la kutilia mkazo namna ya kutunza ndoa. Nyimbo hizo zinaonesha kunga iliomo katika ndoa ambayo baadhi ya watu hawaelewi siri ya maisha ya ndoa. Katika wimbo namba moja (1), wimbo wa *Siri* tunasimuliwa hivi:

Kakae mama kakae, kakae na muumeo
Siri ya nyumba ni mbili, kupata au kukosa

Katika kusawiri nafasi ya mwanamke katika maisha ya ndoa wanawake wanatakiwa kuwa wavumilivu katika maisha yao. Kwani, kama tunavyodokezewa katika wimbo huo hapo juu, "Siri ya nyumba ni mbili, kupata au kukosa" wanawake wanafunzwa kuwavumilia wanaume katika masuala ya kipato. Aidha, katika wimbo namba mbili

(2), wimbo wa *Kigumu* unagusia namna ya kumtunza muume katika ndoa kwa kueleza hivi:

Kigumu mwari kigumu
Kina mrema
Kina mrema aeee kina mrema
Mume ataka tunzwa kina mrema
Tena ataka kupambwa
Kina mrema
Kwa mkadi na waridi
Kina mrema aeee kina mrema.

Wimbo huu unaonesha namna unavyomtaka mwanamke kuhakikisha amemtunza muume wake ili kuendeleza uhusiano bora wa ndoa. Kwa ujumla haya ni mawazo ya jamii ambayo inafuata mfumo dume ambao unawafanya wanawake wawe chini ya wanaume. Mfumo huo unawapa hadhi kubwa wanaume katika baadhi ya mambo kama vile mahusiano ya ndoa. Hiki ndicho pia kinachojidhihirisha katika jamii ya Kiuyu Maambani.

### 4.1.6 Nyimbo Zinazoendeleza Utamaduni

Khamis (2016) anaeleza kuwa dhana ya utamaduni ni jumla ya maisha ya watu katika jamii au jumuia zao katika hali ya kutumia mawazo na vitu katika mazingira yao. Maisha hayo ni pamoja na vipengele vya utamaduni kama mila, silka, desturi, imani, itikadi na jadi za watu katika mazingira yao mahususi ya nchi yao. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa zipo baadhi ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ambazo zinaweza kuekwa katika kundi la nyimbo zinazojadili masuala ya utamaduni wa jamii hiyo. Kwa mfano, wimbo namba kumi (10), wimbo

wa *Mrombo* unaendeleza utamaduni wa kuhudhuria katika taasisi ya unyago. Wimbo huo unasimuliwa hivi:

Mrombo
Nami ni mrombo nisingali kuja
Nami ni mrombo nisingali kuja
Ni mrombo na somo yangu

Katika wimbo huu kunaelezwa suala la miiko ya kuhudhuria katika shughuli ya kutolewa mafunzo ya unyago yanayoambatana na nyimbo za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani. Mtafitiwa baada ya kuimba wimbo huu alieleza kuwa katika jamii ya Kiuyu Maambani kwamba mwanamke amabaye yeye binafsi hakupata mafunzo ya unyago hapaswi kuhudhuria kushiriki kutoa mafunzo ya unyago ya wanawake wengine. Wimbo mwengine unaojadili suala la utamaduni ni wimbo namba kumi na tano (15), wimbo wa *Kituri* ambao unaeleza:

Mwakituri eeee mwakituri turia hapa
Mwakituri eeee mwakituri turia hapa
Mwakituri eeee mwakituri turia hapa

Katika wimbo huu mwanamke anahimizwa kutulia ili kulinda ndoa yake. Utamaduni wa jamii ya Kiuyu Mambani unamtaka mwanamke aliyemo katika ndoa kutulia nyumbani na asitoke isipokuwa pale atapopata ruhusa kutoka kwa muume wake. Vyenginevyo anapotoka bila ya ruhusa ya mume anaonekana amekengeusha maadili ya utamaduni wa jamii hiyo.

Mtafiti kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji aliweza kuzibainisha nyimbo hizi katika kategoria mbalimbali kama zilivyobainishwa katika sehemu hii. Hili lilifanyika kwa kutumia uhusiano wa kile kinachojadiliwa katika nyimbo moja na

nyengine. Hivyo basi, kwa kutumia msimbo unaompa nafasi mhakiki kuihukumu kazi ya fasihi kutokana na uzoefu wa jamii aliweza kuzibainisha nyimbo hizo katika matapo kama yaliyobainishwa hapo juu. Kufanya hivyo kumemfanya mtafiti aweze kulifikia lengo mahususi la kwanza la utafiti huu ambalo lilijikita kubainisha nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani.

## 4.2 Dhamira za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha dhamira katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti amefanya uchambuzi wa dhamira katika nyimbo za nyiso za jamii hiyo. Wamitila (2000) anaeleza kwamba watunzi wa kazi za fasihi ni watu ambao huyachukuwa matukio na visa vinavyotokea katika jamii zao na kuviwakilisha kiubunifu katika hadithi, natiki, hadithi fupi na ushairi. Hivyo uchambuzi wa data zilizokusanywa na mtafiti kutoka kwa watafitiwa zilionesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhamira zifuatazo:

### 4.2.1 Utamaduni

Ramadhani (2013) aneleza kwamba utamaduni ni mfumo au utaratibu wa maisha ambao jamii fulani unaufuata katika maisha ya kila siku ikijumuisha mila, desturi, miiko, matambiko, jando na unyago. Kila jamii ina utamaduni wake kulingana na mazingira ya jamii hiyo. Utamaduni huo unaweza kuangaliwa katika miktadha ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kadhalika. Kwa sababu mielekeo ya maisha hutofautiana kutoka jamii moja na nyengine ni wazi kwamba hata utamaduni wa jamii moja na nyengine umekuwa ukitofautiana na hivyo kuwa na umahasusi kutegemea jamii husika. Hivyo utamaduni wa jamii unaweza kuonekana ni mzuri

kwa wanajamii husika lakini ukaonekana ni mbaya kwa jamii nyengine. Kutokana na ukweli huo data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zimekuwa zikijadili dhamira ya utamaduni kama hali hii inavyojidhihirisha katika wimbo namba kumi (10), wimbo wa *Mrombo* ambapo wimbo huo unaisawiri dhamira hii hivi:

*Nami ni mrombo nisingali kuja*
*Nami ni mrombo nisingali kuja*
*Ni mrombo na somo yangu*

Katika wimbo huu tunaona namna jamii ya Kiuyu Maambani ilivyo na desturi ya kushiriki katika masuala ya mila hasa yanayohusu kuwafundisha watoto wakike kuhusu maadili mema. Hata hivyo, ili kuingia katika kundi la wanaofundisha lazima mtu kwanza awe yeye mwenyewe amewahi kupata mafunzo ya unyago. Wakati wa usaili, watafitiwa walieleza kuwa ni jadi ya jamii hiyo mtu ambaye hakuwekwa kwenye unyago hawezi kushiriki kutoa mafunzo ya unyago wakati wa kutoa mafunzo hayo kwa sababu atakuwa hajui kinachoendelea.

Ingawa ukweli ni kwamba katika jamii ya Kiuyu Maambani wapo wanawake wachache ambao kwa bahati mbaya hawakupita katika mafunzo ya unyago lakini wanachukulia kama na wao ni walimu wa kuwafundisha wanawake wengine kuhusu yale yanayofundishwa katika shughuli za unyago. Hili hutokana na mabadiliko ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ambapo baadhi ya wanawake hujaribu kujifunza masuala yanayohusu maisha ya utamaduni wa mwanamke kupitia mitandao ya intaneti au vyombo vya habari. Hili linajibainisha katika utafiti wa Kalegea (2013) ambaye anaeleza kwamba utandawazi huwafanya watu waige mambo kutoka tamaduni za watu wengine na kuzifanya kuwa ni tamaduni zao.

Aidha, data za utafiti zimebaini kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhamira ya utamaduni wa kumuandaa msichana kutekeleza majukumu ya kazi za familia na hata za uzalishaji mali. Dhamira hii inasawiriwa katika wimbo namba kumi na moja (11), wimbo wa *Mzimu*. Wimbo huo unasimuliwa hivi:

Sona sona sona mzimu sona
Mzimu huu wa nani
Mzimu huu wa tate
Watate wali perere
Waliperere watinya
Tulisake sake
Tulisaure saure
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande.

Watafitiwa walieleza kuwa wimbo huu huimbwa wakati wa mafunzo ya wari ambapo wari hao hupewa mbegu za nafaka kama vile mpunga, mtama, kunde, maharage nakadhalika ili wazioteshe ndani ya wiki mmoja iwe tayari zimeota na kumea vizuri. Wari hao wanatakiwa wazishughulikie kwa kutilia maji asubuhi na jioni ili kuhakikisha kuwa mbegu hizo zimeota na kuchipua vema.

Kitendo cha kuzishughulikia mbegu hizo na kuziotesha vema zinaonesha picha ya namna watakavyoweza kuhudumia shughuli za kilimo pamoja na kushughulikia familia zao pale watakapofunga ndoa. Hivyo kutokana na agizo la kuotesha mbegu za nafaka wari hufanya juhudi na kuhakikisha wamefanikisha maelekezo waliyopewa. Maana yake ni kwamba nyimbo hii ina lengo la kumfanya msichana kuwa mzalishaji kama wanavyofanya wanaume katika jamii hiyo. Ndio maana wanawake wengi wa Kiuyu Maambani wamekuwa wakishiriki katika shughuli za uzalishaji mali hasa

kilimo kutokana na mafunzo waliyopewa wakati wakiwa unyagoni. Ule mpaka wa mgawanyo wa majukumu ya shambani kati ya wanawake na wanaume katika uzalishaji mali ni mdogo sana kati jamii hiyo.

Vile vile, katika wimbo namba kumi na tano (15), wimbo wa *Kituri* tunaibuliwa dhamira ya utamaduni ambapo utamaduni huo unamtaka mwanamke abakie nyumbani kwani yeye ni kiumbe anayestahiki kuwepo katika utawa. Iwapo atatoka katika nyumba yake na kwenda kwenye safari kama zile za uzalishaji mali lazima apate ruhusa kutoka kwa muume wake. Katika wimbo huo tunaelezwa hivi:

Mwakituri eeee mwakituri turia hapa
Mwakituri eeee mwakituri turia hapa
Mwakituri eeee mwakituri turia hapa

Katika wimbo huu msisitizo unaopatikana ni kwamba wanawake waliomo katika ndoa wanapaswa kutii utamaduni wa jamii wa kutokuwa kiguu na njia na hivyo kutii mwiko wa kubakia nyumbani. Mtafiti baada ya kuimba wimbo huu alieleza kuwa kwa kutumia wimbo huu wanawake wanatakiwa wawe katika utawa tangu umri walio hadi pale watapoingia katika ndoa. Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imebainika kwamba tamaduni hizi zimezoeleka katika jamii ya Kiuyu Maambani na kukubalika na jamii hiyo ikiwa ni pamoja na wanawake wenyewe. Utamaduni huu ingawa umekuwa ukikosolewa na baadhi ya wahakiki wa kazi za fasihi kama vile Mulokozi (1999) alipokuwa akifanya uchambuzi wa Utenzi wa Mwanakupona ambapo anaonesha kuwa utenzi huo unamdogesha mwanamke na kumfanya mtumwa wa mwanamme. Pamoja na kuwepo kwa mawazo hayo, jamii hii imechukulia utamaduni wa mwanamke kutulia nyumbani kama utamaduni ambao

unampa hadhi mwanamke huyo. Na kwa sababu hiyo wanawake wenyewe wamekuwa wakitii utamaduni huo.

### 4.2.2 Mapenzi na Ndoa

Mapenzi na ndoa ni taasisi muhimu sana katika jamii za Uswahilini. Kwa sababu ya umuhimu wa taasisi hii, nyimbo za nyiso zimekuwa zikisawiri dhamira ya mapenzi na ndoa. Mafunzo makubwa ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani yanasawiri maisha ya uhusiano wa mapenzi miongoni mwa wanandoa. Katika nyimbo namba moja (1), wimbo wa *Siri* unasawiri dhamira hii moja kwa moja kama ifuatavyo:-

Kakae mama kakae, kakae na mumeo
Siri ya nyumba ni mbili kupata au kukosa

Kupitia wimbo huo tunaoneshwa namna wasichana wanavyopewa mafunzo yanayolenga kujenga uvumilivu katika ndoa zao. Wakati wa usaili watafitiwa walieleza kwamba “watoto wa kike wanaposhiriki katika unyago huimbiwa nyimbo za nyiso ambazo zinawafundisha kuwa katika ndoa kunakuwa na hali ya kupata huduma za kila siku na mara nyengine huweza kujitokeza hali ya kukosekanaa huduma hizo. Hivyo kila mwanandoa anatakiwa azingatie kanuni hiyo ya maisha katika ndoa ili aweze kudumisha maisha yake ya ndoa. Wanawake wengi leo hii wamekuwa si weye subira ya kutosha katika maisha ya ndoa. Wengi miongoni mwao hujikuta wakisimulia ovyo ovyo hali mbaya ya maisha yao wanayoishi ndani ya ndao. Hali hii kwa hakika huwafanya wanandoa kujikuta wakisababisha migogoro mikubwa katika ndoa zao na hatimae ndoa hizo huvunjika kwa sababu wanaume wengi hawapendi kusimuliwa namna hali ngumu

ya maisha ilivyozikabili familia zao. Kupitia nadharia ya Sosholojia kwenye muhimili wake unaohusisha mahusiano ya mwanadamu na jamii yake mafunzo yanayopatikana hapa ni kwamba vijana wanaooana wanatakiwa kujenga na kukuza mashirikiano na mahusiano mema baina yao ili kuimarisha maisha yao ya ndoa. Hii ni kwa sababu kazi kubwa ya muhimili huu ni kujenga uhusiano mwema baina ya mtu na mtu, watu, jamii na taifa kwa ujumla. Wanandoa watakapofikiria kuimarisha uhusiano baina yao kasoro ndogo ndogo zinazoyakabili maisha hazitokuwa kikwazo katika kujenga na kuimarisha ndoa zao.

Aidha, wimbo namba tatu (3), wimbo wa *Pendo* unamuhimiza mwanamke kumtaka aweze kumtosheleza kimapenzi muume wake ili kumuwezesha kufanya kazi kwa bidii. Mawazo haya yanasawiriwa katika wimbo huo kama ifuatavyo:

Ndume hio masikini,
ndume isijeihini
kukicha aenda kazini
mwana msabilie pendo
mwana msabilie pendo

Wimbo huu unamuhimiza mwanamke aliemo katika ndoa kudumisha upendo kwa muume wake ili kuhakikisha ameleta kitulizano kwa muume huyo. Zaidi ya kwamba mwanamke anatakiwa kudumisha mapenzi lakini pia ajue kuwa mwanamme huyo ni maskini hivyo anapaswa kufanya kazi ili kukimu huduma muhimu za familia. Kinyume chake ni kwamba iwapo hatokuwa na mapenzi ya kweli hatoleta kitulizano na matokeo yake mume atakuwa hana utulivu wa kufanya kazi.

Vile vile, katika kujadili dhamira ya mapenzi na ndoa nyimbo za nyiso zinamtaka mwanamke awe tayari kumuhudumia mwanamme na kumtunza. Kufanya hivyo ndio

kunapelekea mapenzi ya kweli na kuleta mvuto kwa wanaume. Katika wimbo namba mbili (2), wimbo wa *Kigumu* dhamira hii inaelezwa kama ifuatavyo:

Kigumu mwari kigumu
Kina mrema
Kina mrema aeee kina mrema
Mume ataka tunzwa kina mrema
Tena ataka kupambwa
Kina mrema
Kwa mkadi na waridi
Kina mrema aeee kina mrema.

Watafitiwa wakati walipohojiwa na mtafiti wa kazi hii walieleza kuwa katika wimbo huo, mwimbaji anamtaka mwanamke ahakikishe amemtunza mwanamme kwa unadhifu ikiwa ni pamoja na kusinga kwa mapambo ya jadi yanayovutia. Mwimbaji analifafanua hili pale anaposema "*tena ataka kupambwa…kwa mkadi na waridi*". lengo lake ni kumtaka mwanamke anapoingia katika ndoa atunze ndoa yake na kuyachapuza mapenzi ya mume kwa kujipamba kwa mapambo kama vile majani ya mkadi; ambayo ni majani maarufu sana katika jamii ya Wapemba ambayo tangu jadi yamekuwa yakitumiwa na wanawake waliomo katika ndoa. Majani haya wanawake huyaweka katika vitanda vyao ili kutoa harufu inayovutia. Aidha, baadhi ya wanawake wa Kipemba hutumia maua ya waridi ili kuleta mvuto na harufu nzuri.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa mafunzo haya ya ndoa na mapenzi ndio msingi mkubwa wa nyimbo za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani ambao hulenga kujenga uhusiano bora katika familia. Kwa ujumla jamii hiyo imekuwa ikiwaweka wanawake katika nyumba maalumu ambazo hupokea mafunzo mbalimbali yanayohusiana na elimu ya jinsia. Katika kupatiwa elimu hiyo

watoto wa kike wanajikuta wakiandaliwa kuwa wanawake bora katika kukabili mapenzi na ndoa pale watakapoingia katika taasisi hiyo. Aidha, kila mwanamke ambaye tayari ameingia katika rika la utu uzima anakuwa na somo yaani mtu ambaye alimpa mafunzo ya unyago. Somo huyo ndie anayechukuwa dhamana ya kumpa mafunzo msichana huyo hadi anaolewa na kwenda kuishi na muume wake. Kwa ujumla somo anabakia kuwa mwalimu wa mwanamke katika masuala ya ujinsia. Mafunzo haya yanasisitiza kutii utamaduni wa jamii hiyo ambao unaaminika hauwezi kupatikana katika taasisi nyengine ya elimu kama vile Skuli na vyuo vya Qurani kupitia walimu wanaosomesha katika taasisi hizo. Hili linasawiriwa pia katika nyimbo za harusi kama utafiti wa Juma (2015) ulivyobaini kuwa nyimbo za harusi katika jamii ya Wapemba ni chuo cha kufunza maadili mema miongoni mwa wanajamii.

### 4.2.3 Usafi

Usafi ni hali ya kutokuwa na uchafu. Usafi ni dhamira nyengine muhimu inayojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Katika nyimbo hizo wanawake wanaoingia katika rika la watu wazima huekwa katika nyumba maalumu na kuimbiwa nyimbo hizo kwa lengo la kuhakikisha wanatunza usafi hasa ule unaohusiana na mwili wao. Katika wimbo namba (4), wimbo wa *Mwari* mwimbaji anaeleza hivi:

Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua
Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua

Katika wimbo huo, mwimbaji anaposema "Mwari wangu chanjaa eee, Chanja mvua," maneno "chanja mvua" ni lahaja ya Kipemba ambayo yanamaana ya "kuoga

maji ya mvua wakati mvua inanyesha.” Kwa kutumia taswira ya “chanja mvua” tunajifunza kwamba wanawake wanatakiwa waoge maji mengi ili kutunza usafi wa mwili wao. Watafitiwa walieleza kuwa usafi ni muhimu sana miongoni mwa wanawake na hujenga heshima na mvuto miongoni mwa wanajamii. Wimbo mwengine unaosawiri dhamira ya usafi ni wimbo namba sita (6), wimbo wa *Ruwanja* ambao unaelezwa hivi:

Mfyagirire mfyagirire ruwanja
Mwenzenu wangweta hao wakifyagira
Mfyagirire aee mfyagirire ruwanja

Katika mfano huo, mwimbaji anasimulia kwa ufupi kuwa pana haja ya kufanya usafi wa kufagia. Hivyo kwa kutumia wimbo huo wanawake wanatakiwa wadumishe usafi ikiwa ni pamoja na kufagia mazingira yaliyowazunguka. Nafasi hii ya kufagia katika jamii ya Kiuyu Maambani kama zilivyojamii nyingi za Afrika imekuwa ikitekelezwa na wanawake. Wanawake hufundishwa kuwa na tabia ya kufanya usafi wa mazingira tangu wanapokuwa wadogo ili watapoingia katika ndoa zao wajue kwamba hiyo ni nafasi ya mwanamke na si ya mwanamme.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji tunabaini kwamba dhamira ya usafi kama inavyojadiliwa katika nyimbo hizi inatoa picha ya maisha halisi ya jamii hiyo ya Kiuyu Maambani. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba jamii hiyo imekuwa ikihimiza usafi miongoni mwa wanajamii. Wanawake wamekuwa wakihimizwa kutunza usafi wa mwili, nguo na hata mazingira yaliyowazunguka. Mathalani, katika jamii hiyo kila asubuhi na jioni wanawake hulazimika kufanya usafi kwa kufagia ndani na nje ya nyumba zao. Hili hufanywa kama ni kanuni ya msingi katika maisha yao ya kila siku. Aidha, katika jamii hiyo hata kifungua kinywa wakati wa asubuhi

hakiwezi kuchukua nafasi iwapo watu katika nyumba husika hawajafanya usafi wa kusafisha vyombo na kufagia nyumba ndani na nje.

### 4.2.4 Uaminifu katika Ndoa

Uaminifu katika ndoa ni dhamira nyengine ambayo inajidhihirisha katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Katika wimbo namba tano (5), wimbo wa *Kiazi* dhamiria hii inasawiriwa hivi:

Kiazi mama kiazi cha nyelele
Kiazi simpi somo, kiazi kinyelele
Kina mafundo mafundo, juu kinaota nywele

Katika ubeti huo, muimbaji anasema “Kiazi simpi somo, kiazi kinyele nyele,” kwa kutumia mbinu hii ya tafsida ambapo neno “kiazi” linalenga sehemu za siri za mwanamke na “somo” ni yule anayetoa mafunzo hayo. Kwa miktadha hii mwanamke anafunzwa kuwa hata mtu wake wa karibu asijaribu kufanya naye ngono holela. Kufanya hivyo kunamfanya mwanamke aonekane ni kiumbe asiye na heshima na aliyekiuka maadili ya jamii hiyo ambayo huhimiza watoto wa kike kuwa wavumilivu kujizuia kufanya ngono holela hadi pale watapofunga ndoa. Watafitiwa walieleza kuwa kufanya uzinzi katika jamii hiyo ni kitendo cha aibu kubwa ambacho humfanya mtu kuonekana hana hadhi na asiyepasa kuheshimika.

Ingawa ukweli wa maisha ni kwamba wanawake wengi leo hii kutoka jamii mbalibali ikiwemo ile ya Kiuyu Maambani wamekuwa wakilalamikiwa kutokana na kutokuwa waaminifu katika masuala ya mapenzi. Hili limekuwa likiibua migogoro miongoni mwa wanafamilia. Mathalani, tunaorejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunabaini kwamba jamii ya Kiuyu Maambani wazazi wa watoto wa kike wamekuwa

na hofu kubwa wakati wa harusi ya mtoto wao kutokana na kutokuwa na uhakika iwapo mtoto huyo atakuwa hajafanya ngono au amefanya kabla ya ndoa yake. Kwani athari ya mtoto wa kike kufanya ngono kabla ya ndoa yake kunapelekea wazazi wake kuonekana hawakufanya juhudi madhubuti katika kumlea mtoto huyo. Pia, mtoto wa kike ambaye amefunga ndoa na kubainika na muume wake kuwa aliwahi kufanya ndoa huweza kumpa talaka na kuivunja ndoa hiyo baada ya kumaliza fungate ya harusi tu, au muume anaweza kuishi naye lakini huku akiwa katika migogoro. Hili la kutokea kwa migogoro kutokana na wanandoa kutokuwa waaminifu linaelezwa pia na Kamau na Buliba (2017) kwamba ni moja ya kichocheo kikubwa cha migogoro katika ndoa.

### 4.2.5 Kuondoa Woga

Woga hutokana na hofu juu ya jambo fulani ambalo mtu hana mazoea nalo. Hivyo utafiti huu ulibaini kwamba nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaibua dhamira ya kuondoa woga miongoni mwa wanawake ambao wanafunga ndoa. Katika wimbo namba kumi na saba (17), wenye kichwa cha habari *Rugumba* anaimbiwa mwanamke ili kumpa picha ya namna maisha ya ndoa yanavyokuwa:

Rugumba eeee
Rugumba eeee
Rugumba kamwambie runyayo
Na runyayo kamwambie sigino
Na sigino umwambie rugoti
Na rugoti umwambie rupaja
Yuwaja aeeee yuwaja aeeee
Yuwaja mgenio yuwaja yuwaja

Wimbo huo, una dhamira ya kumtayarisha msichana ayakabili maisha ya ndoa kimwili na kisaikolojia. Watafitiwa baada ya kuimba wimbo huo wakati wa usaili

walieleza kuwa mwimbaji anaposema "Yuwaja aeeee yuwaja aeeee, yuwaja mgenio yuwaja" anamaana kwamba siku ya kuishi maisha ya ndoa tayari imefika hivyo mwanamke huyo ajue kwamba leo ataanza maisha mapya. Mtafitiwa mmoja alipokuwa akieleza kuhusu dhamira hii ameeleza kuwa ni jadi ya wanawake wa Kiuyu Maambani kuwa na furaha siku hiyo ya ndoa lakini kwa upande mwengine wamekuwa na hofu kubwa kutokana na kuogopa namna watakavyoanza maingiliano ya kimwili jambo ambalo hawajawahi kulifanya hapo kabla. Kwa sababu hiyo wanawake wengi wamekuwa na woga. Hivyo ili kushinda woga huo wanawake wanatakiwa walione ni jambo la kawaida ingawa ni geni. Wimbo mwengine unaosawiri dhamira hii ya kuondoa woga miongoni mwa wanawake ni wimbo namba kumi na sita (16), wenye kichwa cha habari *Mkia wa ngombe*. Katika wimbo huo tunaelezwa hivi:

Kwaja mkia wa ngombe huo
Kwaja mkia wa ngombe huo
Ukienda udama udama
Ukirudi udama udama

Katika wimbo huu kuna matumizi ya kifungu cha maneno "Kwaja mkia wa ngombe huo," ni tafsida inayomaanish "sehemu ya siri ya mwanamme." Kama ilivyoelezwa na mtafiti hapo kabla kwamba dhamira hii ina lengo la kumtayarisha mwanamke awe tayari kuanza maisha mapya ya ndoa yake ambayo sasa maisha hayo yanaruhusu kufanya mapenzi na muume wake. Wimbo huu huimbwa na wale ambao ni watani wa mwanamke ama somo.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo moja ya msingi wa nadharia hii ni kuangalia namna kazi ya fasihi inavyosawiri kile kinachojitokeza

katika jamii tunaweza kusema kuwa nadharia hii imelandana na dhamira ya woga miongoni mwa jamii iliyotafitiwa. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba wanawake wengi wamekuwa wakijizuia kufanya ngono kabla ya kufunga ndoa katika jamii ya Kiuyu Maambani. Kwa sababu hiyo, wanawake wanapofika siku ya kufunga ndoa wanakuwa na hofu ya namna gani wataanza maingiliano ya kimwili. Hivyo jamii imekuwa na tabia ya kuwapa "kungwi," yaani mwanamke ambaye ataambatana na bibi harusi huko anakoenda kuanza maisha mapya. Lengo la kuwepo mwanamke huyu ni kumfundisha maisha ya ndoa kivitendo na kumpa mafunzo ya ziada ya kuondoa ya kukabiliana na maisha hayo.

### 4.2.6 Umoja na Mshikamano

Data zinaonesha kuwa baadhi ya nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaibua dhamira ya umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, wimbo namba tisa (9), wenye kichwa cha habari *Kumekucha* unatuibulia dhamira hii ya umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii kama ifuatavyo:-

Kumekucha eee
Kumekucha kumenanauka
Mwenye tama na atamauke
tupe mamae harusi
Tupe kinura mgongo

Watafitiwa walioimba wimbo huu walieleza kuwa wimbo huo umekuwa ukiimbwa na wanawake majirani wa mama wa mtoto wa kike akiwemo somo wa mtoto wa kike huyo wakati wa asubuhi ya kuamkia siku ya harusi. Wanawake hao huwa wako katika kikundi. Kundi hilo ni picha ya umoja na mshikamano walionao wanawake wa Kiuyu Maambani wakati wa shughuli za harusi za watoto wao. Harusi hizo hubakia

kuwa ni tukio la kijamii ambalo huwaunganisha wanawake wa jamii mzima. Hii ni kaida waliyonayo wanawake wengi wa jamii za Uswahilini. Katika kuelezea umoja huo unaojidhihirisha miongoni mwa Waswahili wakati wa sherehe ya harusi Ali (2015) alipokuwa akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Kiu* anaonesha namna jamii ya Wazanzibar wakiwakilishwa na familia yao Bahati na majirani wao walivyoshirikiana na kuwa wamoja katika sherehe ya harusi ya Bahati na Iddi.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunabaini kwamba suala la umoja na mshikamano kama linavyojitokeza katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani hasa wakati wa sherehe za harusi ndilo linalodhihirika katika jamii hiyo wakati wa harusi. Kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtafiti ya kuhakiki mambo kutokana na uzoefu wake na tajiriba aliyonayo katika jamii, mtafiti amekuja na maoni yasemayo kwamba kupitia unyago ambao huambatana na nyiso wanajamii hushirikiana bila kujali matatizo yaliyopo kati yao. Hata zile familia ambazo zilikuwa na chuki kati yao, au hata wale wenye uhusiano mbaya kati ya mtu mmoja na mwengine ambaye ni mhusika katika tukio hilo, hujikuta chuki hizo zikisahaulika ama kuamua kuziweka pembeni ili kufanikisha jambo hilo. Iwapo jirani ataendeleza mgogoro na kususia kushiriki katika mafunzo hayo ambayo mara nyengine hutolewa wakati wa tukio la harusi inayohusika wanajamii wengine wanamuona kuwa amefanya matendo yasiyo na utu.

### 4.2.7 Umuhimu wa Kazi

Kazi ndio msingi wa maisha ya kila mwanajamii. Jamii yoyote inatakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kupata kipato. Hivyo nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani

zinajadili dhamira ya kazi. Mfano wa wimbo unaosawiri dhamira hii ni wimbo namba kumi na moja (11), wimbo wa *Mzimu* ambapo dhamira hii inasawiriwa hivi:

Sona sona sona mzimu sona
Mzimu huu wa nani
Mzimu huu wa tate
Watate wali perere
Waliperere watinya
Tulisake sake
Tulisaure saure
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande

Katika wimbo huu tunaoneshwa namna suala la kazi linavyotiliwa mkazo miongoni mwa wanajamii bila ya kujali jinsia. Kupitia wimbo huu watoto wanatayarishwa kuwa wazalishaji na washiriki katika kilimo. Katika wimbo huo, wasichana wanapoimbiwa "Nyikanga hao tuwape mbeu wapande" muimbaji analengo la kuwafanya washiriki katika uzalishaji mali. Kutokana na utamaduni huo wa kuwataka wanawake washiriki katika shughuli za uzalishaji mali, ndio maana wanawake hao wamekuwa ni wazalishaji mali.

Kwa ujumla tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kwa kutumia msingi wa kuiangalia kazi ya fasihi na namna mhakiki atakavyoihukumu kutokana na yale yanayojitokeza katika jamii tunabaini kuwa jamii ya Kiuyu Maambani wanawake wamekuwa wakishiriki katika uzalishaji mali hasa katika kilimo. Wanawake hao wamekuwa wakizalisha mazao ya shambani kama vile mpunga, njugu, kunde, mahindi na tungule. Kwa ujumla kilimo cha tungule kimekuwa kikiwapatia mapato makubwa ambayo baadhi yao wameweza kujikimu kwa kupata huduma muhimu za

kijamii kama vile chakula na hata kujenga nymba za kuishi baada ya mavuno yao na kuyauza sokoni.

## 4.3 Dhima Katika Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu limejikita kuchunguza dhima za nyiso katika jamii ya Kiuyu Maambani. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina nafasi muhimu katika jamii kutokana na kuwa na dhima mbalimbali. Utafiti huu umebaini kuwa pamoja na nyimbo za nyiso za jamii hiyo kujikita kutoa mafunzo kwa wanawake wanaokuwa unyagoni lakini dhima zake zinaigusa jamii katika vipengele mbalimbali vya maisha. Dhima hizo ni kama zifuatavyo:-

### 4.3.1 Kukuza Mshikamano katia Jamii

Wakati wa kufanya usaili, watafitiwa walieleza kuwa dhima moja muhimu ya nyiso za jamii hiyo ni kukuza mashirikiano miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, wimbo namba tisa (9), wimbo wa Kumekucha ulielezwa kuwa umekuwa ukiwahamasisha wanawake kuwa pamoja katika shughuli za kijamii kama vile harusi. Wimbo huu unaeleza hivi:

> Kumekucha eee
> Kumekucha kumenanauka
> Mwenyetananaatamauke
> tupe mamae harusi
> Tupe kinura mgongo

Watafitiwa wakati wa usaili walieleza kuwa wimbo huo huimbwa asubuhi ya kuamkia siku ya harusi ya mtoto wa kike. Wanawake ambao walikaa na bibi harusi usiku wote wakimfundisha masuala ya ndoa kama vile namna ya kuishi vema na

muume, namna ya kushiriki katika mapenzi na muume wake, namna ya kuhudumia nyumba pamoja na namna ya kuishi na ndugu wa muume wake ikiwamo shemegi zake hutoka kwa pamoja na kumfuata mama mzazi wa mwanamke atakae olewa wakiimba nyimbo hiyo kama ishara ya kuonesha umoja wao kwamba wamemaliza kumfundisha mtoto wake hivyo wanahitaji kinura mgongo yaani asante. Utamaduni huu umeenea sana katika jamii za Uswahilini ndio maana hata Mohamed Suleiman katika riwaya ya *Kiu* anaisawiri ndoa ya Bahati na Iddi namna majirani walivyoshiriki kwa pamoja katika kufanikisha ndoa hiyo.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo imetumika katika kumuongoza mtafiti imedhihirisha kuwa zipo nyimbo za nyiso zenye jukumu la kuwaunganisha wanajamii wa Kiuyu Maambani hasa katika shughuli zinazoambatana na sherehe za unyago. Katika jamii hii wakati wa kutoa mafunzo hayo kila mmoja huungana na mwengine ili kuhakikisha kuwa wamefanikisha kumuandaa mtoto wa jirani au ndugu yao. Mafunzo haya hutolewa na wanawake tu wanaume wao hawashiriki. Aidha, katika jamii hii suala la mafunzo ya unyago huendelea hadi mtoto anaolewa na kufungamanishwa na familia ya muume wake. Hii ni kusema kuwa unyago wa jamii ya Kiuyu Maambani ni tukio endelevu na halimalizii wakati wa kuingia katika rika la watu wazima tu.

### 4.3.2 Kuhimiza Ustahamilivu

Kutokana na uhalisia wa maisha ya jamii yaliyomo katika maisha ya wanandoa, nyimbo za nyiso hutumika kujenga ushujaa na ustahamilivu katika maisha ya ndoa miongoni mwa wanawake. Baadhi ya watafitiwa walieleza kuwa nyimbo za nyiso ni asasi muhimu sana kwa wanawake ambao bado wanauelewa mdogo kuhusiana na

ukweli kuhusu maisha. Kwa mfano, katika wimbo namba moja (1), wimbo wa *Siri* dhima hii inasawiriwa hivi:

Kakae mama kakae, kakae na mumeo
Siri ya nyumba ni mbili kupata au kukosa

Wimbo huo huwapa wanawake nafasi ya kutafakari kuhusiana na hali ya maisha atayokutana nayo katika maisha ya ndoa ambayo ataingia hapo baadaye. Aidha, nyiso huwajenga ushuja wanawake kuwa wastahamilivu katika kukabiliana na changamoto za maisha. Mifano ya changamoto hizo ni kama vile kupata au kutopata mlo wa kutwa, kupata huduma za vivazi anavyoona kuwa vinafaa. Mwanamke huyo anatakiwa awe mstahamilivu ili kuendeleza ndoa yake iwapo kwa bahati mbaya atakumbana na changamoto hizo atapoingia katika uhusiano wa ndoa. Wanawake wengi wanatakiwa kulijua hilo kutokana na watu wengi leo hii kutototosheka na kile wanachokipata ndio maana katika wimbo huo mwanamke anaelezwa kuwa “Siri ya nyumba ni kupata au kukosa”. Baadhi ya wanawake wamejaa tamaa ya kutaka kuishi maisha ya kifahari. Matokeo yake kwa vile baadhi ya wanaume huwa hawamudu gharama hizo kunaibuka mgogoro na hatimae kupelekea kuvunjika kwa ndoa yao.

Kitu kingine cha msingi ambacho kinahimizwa kuwa na ustahamilivu ni suala zima la kuishi katika mahusiano ya ndoa. Falsafa ya jamii ya Kiuyu Maambani ni kwamba mwanamke anapaswa kumuhudumia mwanamme. Hali hii inaelezwa kwenye wimbo namba mbili (2), wimbo wa *Kigumu* ambao unaeleza hivi:

Kigumu mwari kigumu
Kina mrema
Kina mrema aeee kina mrema
Mume ataka tunzwa kina mrema

Tena ataka kupambwa
Kina mrema
Kwa mkadi na waridi
Kina mrema aeee kina mrema.

Katika wimbo huo, dhima ya kuwajenga wanawake kuwa na uvumilivu katika ndoa zao inabainika. Dhima hii kwa kiasi kikubwa inalenga kumtayarisha mwanamke kuwa mvumilivu kwani asasi ya ndoa katika jamii ya Kiuyu Maambani ina miiko yake ya kumtaka mwanamke ahakikishe amemuhudumia mwanamme ili aweze kufurahia maisha ya ndoa ndio maana katika nyimbo hiyo tunaelezwa "Muume ataka tunzwa kina mrema." Pia, mwanamme anahitaji kudumishiwa usafi ambao utalenga kuongeza mvuto katika ndoa hiyo. Nafasi aliyonayo mwanamme kukamilisha dhima hiyo ni kufanya juhudi za kutimiza mahitaji yanayoambatana na matunzo hayo kama vile ununuzi wa mapambo.

Kwa hivyo kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kwamba dhima ya kuhimiza uvumilivu kama inavyojidhihirisha katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani inasawiri uhalisia wa maisha ya jamii hiyo katika suala linalohusu elimu ya uhusiano wa ndoa miongoni mwa wanandoa. Ukweli ni kwamba maisha ya wanandoa katika jamii hii ni yale tunayoweza kusema kuwa ni maisha ya uvumilivu na yanayompa mwanamme hadhi kubwa kuliko mwanamke kama zilivyo jamii nyingi ambazo zina mfumo dume. Aidha, katika jamii hii wapo wanandoa wanaishi katika hali ya kupata au kukosa hata hivyo wanandoa hao wanaendelea kuvumiliana ili kuendeleza uhusiano wao wa ndoa.

### 4.3.3 Kubainisha Utamaduni wa Jamii

Kila jamii ina mila, desturi na utamaduni wake. Utamaduni ni nyenzo muhimu ya utambulisho wa jamii husika (Hassan, 2017). Kwa hivyo, data zinaonesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinasawiri utamaduni wa jamii hiyo. Hii ni kusema kwamba nyimbo za nyiso zina dhima ya kuonesha utamaduni wa jamii husika. Katika wimbo namba saba (7), wimbo wa *Kigugusi* tunaelezwa namna utamaduni wa jamii hiyo unavyowataka wanawake wasijitokeze mbele ya wageni wanaume. Utamaduni huo unaelezwa hivi:

Kigugusi amwambia unyayo
Ukatazwalo ndilo ufanyalo
Mgeni wetu wajana na leo kaja

Katika wimbo huo, neno "kigugusi" ni neno la lahaja ya Kiswahili cha Kipemba ambalo lina maana ya mtu mkaidi au asiesikiliza maelekezo anayoambiwa ingawa yana manufaa naye. Aidha, neno hilo mara nyengine huwa na maana ya mwanamke anayependa kwenda huku na kule. Hivyo katika wimbo huo mwanamke anatakiwa asiwe na tabia ya kufanya ukaidi, asikie anayoambiwa na aache kwenda kule na huku hasa kujionesha mbele ya wanaume. Kufanya hivyo huchukuliwa kuwa ni utamaduni ambao haukubaliki miongoni mwa wanawake wa jamii ya Kiuyu Maambani. Kutokana na utamaduni huu ndio maana wanawake wengi wamekuwa wakiwakimbia wanaume ambao ni wageni kwa sababu ya kulinda utamaduni huo. Msailiwa mmoja alieleza kwamba hata kutaka kutafuta mchumba wa kufunga naye ndoa katika jamii ya Kiuyu Maambani mara nyengine inakuwa ni vigumu kwa mwanamme ambaye ni mgeni kwa vile wasichana hao wanaposikia kuna mwanamme ambaye ni mgeni hukimbia na kujificha vyumbani mwao hadi pale mzazi au mtu wanaemuheshimu

kama mwalimu wa shule, mwalimu wa chuo cha Qur-ani anapowaita mbele ya wageni hao wanaweza kutoka na kwenda. Hivyo hii ndio mbinu ambayo hufanywa na wale wanaotaka kuwaona wanawake wa jamii hii iwapo wanachagua mchumba. Ingawa miiko hiyo ya utamaduni huweza kukengeushwa wakati wa shughuli muhimu kama vile sherehe za Iddi na harusi wasichana unaweza kuwaona mitaani.

Utamaduni mwengine unajidhihirisha katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ni utamaduni unaohusu miiko ya mwanamke kumuelezea mtu mwengine kuwa ameingia katika siku zake. Kwa jamii hii kulieleza wazi wazi suala hilo ni kuvunja utamaduni wa jamii hiyo. Kwa mfano, katika wimbo namba nane (8), wimbo wa *Wageni* tunasimuliwa kwa njia ya kishairi hivi:

Pano pakanja kujiri wageni
Pano pakanja kujiri wageni
Kujiri wageni kujiri wageni

Katika wimbo huo, kuna matumizi ya tafsida "Kujiri wageni" ambapo inalengo la kumuelezea mwanamke akiwa katika mzunguko wake wa siku kimwili. Matumizi haya ya tafsida yanatumiwa ili kuwazoesha wanawake kutozungumzia suala hilo mbele ya jamii na hivyo kutakiwa iwe ni siri. Kwa jamii ya Kiuyu Maambani wanawake wanaposema kunakuja wageni wao wanajua maana iliyokusudiwa hata hivyo neno hilo pia huwa halizungumzwi kila mara kwani huchukuliwa kama ni kumdhalilisha mwanamke.

Wimbo mwengine uliobainisha dhima ya utamaduni wa Kiuyu Maambani ni wimbo namba kumi na mbili (12), wimbo wa *Somo*. Katika wimbo huo tunaelezwa namna

jamii hiyo ilivyo na utamaduni wa kutumia nyiso kama ni chuo cha kutoa mafunzo miongoni mwa wasichana. Katika wimbo huo tunaelezwa hivi:

Nawa nawa somo yangu nikwambie
Ikiwa kuna makosa somo nikuangukie
Kuna hadithi za wari somo nikuhadithie
Na waee nawaee somo
Tumbo langu lina njawaa

Katika wimbo huo, mtafitiwa alipokuwa akifanyiwa usaili alieleza kuwa una dhima ya kuonesha utamaduni wa msichana kuhusiana na wanawake kuvunja ukimya. Kwa kawaida wasichana hao wanapokabiliwa na tatizo ambalo linakwamisha ustawi wa maisha yao au afya zao kama vile magonjwa ya kina mama, tatizo la kujikuta katika mapenzi ya umri mdogo, kunyanyapaliwa, nakadhalika wanamueleza somo ili kupata ushauri. Utamaduni huu unamfanya somo kuwa ndie mwenye dhamana ya kujua siri ya mtoto wa kike ambaye alipewa kumpa mafunzo. Somo ni kiwakilishi cha mwanamke ambaye amechukua jukumu la kumfundisha mtoto wa kike elimu ya ujinsia katika jamii ya Wapemba.

Aidha, nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaonesha dhima ya utamaduni wa kumtunza mwanamme ili kujenga uhusiano wa ndoa ulio bora. Nyimbo ambayo inasawiri dhima hii ni wimbo namba mbili (2), wimbo wa *Kigumu* unasawiri utamaduni wajamii kuhusiana na mahusiano ya ndoa kwa kusema:

Kigumu mwari kigumu
Kina mrema
Kina mrema aeee kina mrema
Mume ataka tunzwa kina mrema
Tena ataka kupambwa

Kina mrema
Kwa mkadi na waridi
Kina mrema aeee kina mrema.

Suala la mwanamke kuhakikisha anamtunza mume kutokana na mapambo mbalimbali ya kijadi kama vile mkadi na waridi ni utamaduni unaosawiriwa katika nyimbo hii. Watafitiwa waliouimba wimbo huu walieleza kuwa nyimbo hii huimbiwa wanawake ambao wamewekwa ndani siku tatu kabla ya kufunga ndoa. Siku hizo tatu wanakuwa wamewekwa ndani ya nyumba ya jirani ambapo somo, dada na ndugu wa karibu wanamuimbia nyimbo hii ili ajue kuwa usafi wa mwanamme unategemea zaidi mwanamke. Kwa msingi huo, wanawake wanalazimika kufua nguo za muume wake, kumuwekea muume maji ya kuoga kila asubuhi na jioni na pale anaporudi kazini. Nafasi hiyo inakuwa ni ya mwanamke na iwapo hatoitekeleza mwanamke huyo anahesabiwa na wanajamii kama ni mwenye kukengeuka utamaduni kuhusiana na ndoa yake. Utamaduni huu unakubaliwa na wanawake wenyewe pamoja na jamii hiyo. Katika mtazamo wa ujinsia Wanawake hao binafasi hawaoni kuwa wanakandamizwa. Ingawa wapo baadhi ya wahakiki ambao wanakosoa utamaduni huo. Kwa mfano, Mulokozi (1999) alipokuwa akifanya uchambuzi wa *Utenzi wa Mwanakupona* anakosoa utamaduni wa kumfanya mwanamke ajitunze kwa ajili ya mwanamme akidai kuwa huko ni kumkandamiza mwanamke.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama inavyoelezwa na Wafula (2007) tunaona kuwa suala la utamaduni kama linavyoelezwa katika nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani linaendana na uhalisia wa maisha ya jamii hiyo. Wanawake wamekuwa wakitoa elimu ya jinsia kupitia nyimbo za nyiso ambazo hutoa maelekezo na mafunzo kuhusu masuala ya utamaduni wa jamii hiyo.

### 4.3.4 Kuhimiza Ujasiriamali

Ujasiriamali ni shughuli ambazo huwafanya watu waweze kujitigemea katika kuyakabili maisha badala ya kutegemea kuajiriwa na watu wengine. Hii ni taasisi ambayo inamfanya mtu ajiajiri. Data zilizokusanywa zinaonesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima ya kuhimiza vijana kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali hasa katika shughuli za kilimo. Wimbo namba kumi na moja (11), wimbo wa *Mzimu* unalieleza hilo hivi:

Sona sona sona mzimu sona
Mzimu huu wa nani
Mzimu huu wa tate
Watate wali perere
Waliperere watinya
Tulisake sake
Tulisaure saure
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande
Nyikanga hao tuwape mbeu wapande

Kupitia nyimbo za nyiso za jamii hiyo wari wanafunzwa kufanya kazi kwa bidii. Katika wimbo huo mwimbaji anaposema “Nyikanga hao tuwape mbeu wapande” lengo lake ni kuwaweka vijana kufanya bidii katika kazi. Muimbaji wa nyimbo hii wakati wa usaili alimueleza mtafiti kuwa wale wanaokuwa katika unyago hupewa mbegu za nafaka kama vile mpunga, mahindi, kunde, njugu na maharage ili wazioteshe na kuzishughulikia ndani ya wiki moja. Katika kuziotesha wanalazimika wazimwagilie maji na kuzishughulikia vema ili ziweze kustawi.

Tukio hili huwafanya watoto kukua na fani maalumu za kilimo zinazoweza kuwasaidia kimaisha. Mtoto anaweza kuwa na ujuzi fulani kuhusu kilimo ambacho

alikipata wakati wa shughuli za unyago. Kwa mkabala huu tunaona kuwa nyimbo za nyiso zinakuwa ni asasi ya kumshirikisha mwanamke katika uzalishaji mali.

### 4.3.5 Kufundisha Maadili Mema

Maadili mema ni tabia zinazokubalika katika jamii, tabia hizo huwa ni muendelezo wa urithi uliopatikana tokea kizazi hadi kizazi. Hassan (2017) anaeleza kuwa maadili ni sawa na tabia zilizomzuri katika jamii. Data zilizokusanywa zinaonesha kwamba nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinadhima ya kurithisha maadili mema ya jamii. Utafiti umebaini kuwa kupitia nyimbo hizo, watoto hufunzwa adabu na kaida za jamii ili wafanye yanayokubalika na kuaswa yale yasiyokubalika na jamii. Dhima hii inajitokeza katika wimbo namba nne (4), wimbo wa *Mwari* ambapo mtoto wa kike anahimizwa kutunza usafi wa mwili wake. Wimbo huo unaeleza hivi:

Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua
Mwari wangu chanjaa eee
Chanja mvua

Katika wimbo huo, kuna matumizi ya fungu la maneno linaloeleza "Mwari wangu chanja eee, Chanja mvua." Neno "kuchanja" ni neno lenye asili ya lahaja ya Kipemba lina maana ya kuoga hasa kwa kutumia maji ya mvua wakati inaponyesha. Katika jamii hiyo, watoto huoga huku wakiwa wamevaa nguo zao. Hivyo kwa kutumia wimbo huu, watoto wa kike hutakiwa wasafishe miili yao pamoja na nguo zao ili kutunza usafi. Zaidi ya hayo nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima ya kutunza siri hasa kwa mambo yanayohusu masuala ya mabadiliko ya mwili wa mwanamke. Kwa mfano, wimbo namba nane (8), wimbo wa *Wageni* unasawiri dhima hii hivi:

Pano pakanja kujiri wageni
Pano pakanja kujiri wageni
Kujiri wageni kujiri wageni

Katika wimbo huo kuna matumizi ya maneno "Kujiri wageni," lenye maana ya tafsida ya mwanamke kuingia katika siku zake. Baada ya kuimba wimbo huo, mtafitiwa wakati alipokuwa akifanya usaili na mtafiti alieleza kuwa wimbo huu unatumika kwa lengo la kuwajenga maadili watoto wa kike ambao wanaingia katika siku zao wasithubutu kueleza kitendo hicho wazi wazi na badala yake wanaweza kutumia kifungu cha maneno "wageni." Kwa ujumla katika jamii hiyo suala la mwanamke kuingia katika siku zake linatunzwa kuwa ni siri kubwa miongoni mwa wanajamii. Aidha, kulieleza suala hilo mbele ya wanaume huchukuliwa kuwa ni kitendo cha aibu miongoni mwa wanawake.

Dhima hii ya maadili pia inaonekana katika wimbo namba moja (1), wimbo wa *Siri*. Ambapo katika wimbo huo mwanamke anatakiwa awe na tabia ya kutunza siri ya maisha yake katika uhusiano wa ndoa. Kwa mfano, katika wimbo huo tunaelezwa hivi:

Kakae mama kakae, kakae na mumeo
Siri ya nyumba ni mbili kupata au kukosa

Mtafiti alipofanya usaili na mtafitiwa alielezwa kuwa wimbo huo umekuwa ukiimbiwa watoto wa kike ili kujenga maadili mema yanayohusu maisha ya uhusiano wa ndoa. Mtafitiwa alieleza kuwa wapo baadhi ya wanawake baada ya kufunga ndoa wanataka wapate kila wanachokitaka kutoka kwa muume jambo ambalo mara nyengine huwa jukumu hilo haliwezi kutekelezeka kutokana na hali halisi ya maisha

ya jamii zetu pamoja na vipato vya baadhi ya wanaume. Hivyo, wanawake hao wanatakiwa walijuwe hilo kabla ya kufunga ndoa zao.

Aidha, katika wimbo namba kumi (10), wimbo wa *Mrombo* unaeleza maadili ya wanawake kushiriki katika kutoa mafunzo dhidi ya wanawake wengine. Mrombo ni mtu ambaye anajua kuhusu masuala ya unyago. Katika wimbo huo tunaelezwa hivi:

> Mrombo
> Nami ni mrombo nisingali kuja
> Nami ni mrombo nisingali kuja
> Ni mrombo na somo yangu

Wimbo huu ni mmoja kati ya wimbo ambao umekuwa ukifunza maadili ya jamii ya Kiuyu Maambani. Baada ya kuimba wimbo huo mtafitiwa alimueleza mtafiti kuwa maadili ya jamii hayamruhusu mwanamke ambaye hakuwahi kukaa unyagoni kushiriki katika kutoa mafunzo ya watoto wa kike wanapokuwa katika unyago. Hii ni kusema kuwa lazima anayetoa mafunzo ya unyago awe na yeye amewahi kukaa na kupatiwa mafunzo katika unyago. Vyenginevyo iwapo mwanamke huyo atatoa mafunzo anachukuliwa kama ni mkengeushi wa maadili. Aidha, mtafitiwa alieleza kuwa mwanaume ijapokuwa anauelewa fulani wa namna ya kuwafundisha wari hawezi kushiriki katika kuimba nyimbo za nyiso kwa minajili ya kuadilisha jamii hiyo kwa sababu suala hilo linawahusu wanawake wenyewe tu.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiiti anaweza kueleza kuwa dhima inayohusu maadili ndio msingi wa nyimbo za nyiso katika jamii iliyotafitiwa kama zilivyo nyiso za jamii nyengine hapa Afrika. Hili linaungwa mkono na Ndungo na Wafula (1993) ambao wanaeleza kuwa nyimbo za jando na unyago zina dhima kuu ya kuifunza jamii maadili ya tohara na kuwa mtu mzima.

### 4.3.6 Kuburudisha

Moja ya dhima muhimu ya kazi ya fasihi ni kuburudisha wanajamii. Kwa sababu hiyo hata nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima ya kuburudisha jamii. Karibu nyimbo zote zilizofanyiwa utafiti zinadhihirika kuwa ni kichocheo cha kuibua burudani kwa hadhira. Mfano wa wimbo ambao unatumiwa na jamii kama ni burudani ni wimbo namba kumi na saba (17), wenye kichwa cha habari *Rugumba* ambao unaeleza hivi:

Rugumba eeee
Rugumba eeee
Rugumba kamwambie runyayo
Na runyayo kamwambie sigino
Na sigino umwambie rugoti
Na rugoti umwambie rupaja
Yuwaja aeeeeyuwaja aeeee
Yuwaja mgenio yuwaja yuwaja

Mtafiti wakati alipokuwa akifanya usaili na mtafitiwa alieleza kuwa wimbo huu pamoja na mambo mengine hutumiwa katika unyago kama sehemu ya kuburudisha wari hasa pale anapopatikana muimbaji manju mwenye sauti nyororo na ya kuvutia. Kutokana na burudani hiyo wanawake hujikuta wakicheza kwa pamoja na kushereheka kwa pamoja. Mfano mwengine wa wimbo wa nyiso unaotumika kama sehemu ya burudani miongoni mwa hadhira ni wimbo namba kumi na nne (14), wenye kichwa cha habari *Pamrango* ambao unaimbwa hivi:

Pamrango
Pamrango parindata ndata
Pari ndata ndata
Pamrango parindata parindata ndata

Upate ndira upite
Paripotata ritataure tataa
Paripotata ritataure tataa
Upate ndira upite

Aidha, mtafitiwa baada ya kuimba wimbo huu alimueleza mtafiti kwamba wimbo huu huwa unaimbwa na hadhira kwa pamoja huku midundo ya ngoma ikiambatanishwa pamoja na vigelegele ili kuchapuza wimbo huu. Kutokana na wimbo huu waimbaji na hadhira hujikuta wakiburudika kwa pamoja. Dhima hii ya kuburudisha inalandana na nadharia ya Mwitiko kutokana na ukweli kwamba katika jamii yoyote nyimbo kama sehemu ya fasihi hutumika kuiburudisha hadhira kama hili linavyoelezwa na Ndungo na Wafula (1993) kwamba baadhi ya nyimbo za jando na unyago hutumika kuwaburudisha wari.

## 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii ya nne imebainisha data zilizokusanywa ambazo zililenga kujibu maswali ya utafiti huu. Sura hii ina sehemu tatu ambapo sehemu ya kwanza inabainisha aina za nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Sehemu ya pili imefafanua dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani na sehemu ya tatu imefanya uwasilishaji wa data za utafiti zinazohusu dhima za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Kwa ujumla sura hii imeweza kuyafikia malengo ya utafiti huu. Hivyo sura inayofuata inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ametoa muhutasari, hitimisho na mapendekezo. Sura hii ina sehemu tatu. Sehemu ya kwanza imebeba muhtasari wa tasnifu hii, sehemu ya pili inaelezea matokeo ya utafiti na sehemu ya tatu inaeleza mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhutasari wa Tasinifu

Utafiti huu ulikuwa na lengo la Kuchunguza nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Nyimbo zilizofanyiwa utafiti ni zile ambazo zimekuwa zikiimbiwa wari wakati wa unyago au wakati wa sherehe ya harusi katika jamii hiyo.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni; Kubainisha nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; `Ni zipi nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani? Lengo mahususi la pili lilikuwa ni Kueleza dhamira katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "Ni dhamira zipi zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani?" Na lengo mahususi la tatu lilikuwa ni "Kufafanua dhima za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani." Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "Nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima zipi?"

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi ya utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amebainisha na kueleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu na

malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu hii.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura hii inasehemu ya utangulizi, dhana muhimu katika utafiti huu ambazo ni utangulizi wa sura, dhana ya nyimbo, dhana dhamira, dhima za fasihi na mapitio ya maandiko kuhusu nyimbo. Aidha, sura hiyo inabainisha pengo la utafiti huu. Mwisho sura hii imeeleza nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo imeongoza utafiti huu.

Katika sura ya tatu, utafiti umeelezea mbinu na vifaa vilivyotumika kukusanya data za utafiti huu. Vipengele vilivyoelezwa katika sura hii ni usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na walengwa wa utafiti. Vipengele vyengine ni sampuli na mbinu za usampulishaji. Pia, sura hii inaelezea data na aina za data, mbinu za ukusanyaji data na uchambuzi wa data.

Sura ya nne imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo tatu. Sehemu hizo zimepangwa kutegemea malengo mahususi ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imewasilisha data za utafiti zinazohusu kubainisha nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Sehemu ya pili inahusu uwasilishaji wa data zinazohusu dhamira zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani na Sehemu ya tatu imewasilisha dhima za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Mwisho, sura imetoa hitimisho.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhutasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Sura hii inaeleza kwa muhtasari kile kilichogunduliwa na mtafiti. Maswali yote matatu yaliyoongoza utafiti huu yanaelezwa majibu yake kwa ufupi

kama ilivyobainishwa na kugunduliwa katika sura ya nne ya tasnifu hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Hivyo uchambuzi wa data umetoa matokeo ya utafiti huu kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha nyiso zinazopatikana katika jamii ya Kiuyu Maambani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti la kwanza lisemalo: "Ni zipi nyiso zinazopatikana katika jamii ya Kiuyu Maambani?"

Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kwa kutumia kigezo cha dhima, nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zinaweza kuwekwa katika makundi ya nyimbo zinazofunza usafi, nyimbo zinazokuza umoja na mshikamano, nyimbo zenye kuonya, nyimbo zenye kuhamasisha kazi, nyimbo zinazofunza maisha ya ndoa na nyimbo zinazoendeleza utamaduni wa jamii.

### 5.3.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: "Kueleza dhamira zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "Ni dhamira zipi zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani? Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa dhamira zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani ni dhamira ya utamaduni, mapenzi na ndoa, usafi, uaminifu katika ndoa, kuondoa woga, umoja na mshikamano na dhamira ya kazi.

### 5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni: “Kufafanua dhima za nyiso zinazoimbwa katika jamii ya Kiuyu Maambani” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni dhima zipi zinazopatikana katika nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani?” Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zina dhima za kukuza mshikamano katika jamii, kuhimiza usatahamilivu, kubainisha utamaduni wa jamii, kuhimiza ujasiri amali, kufundisha maadili mema na kuburudisha.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhima za nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Kwa ujumla mtafiti aligundua kuwa nyimbo za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani zimekuwa na dhima kadhaa ambazo zinahusu maisha ya ndoa pamoja na maisha ya kila siku kama vile kuhimiza kazi, kuonesha utamaduni nakadhalika. Hivyo basi, utafiti huu umegundua kuwa nyimbo za nyiso ni chuo cha kuwafunza maisha wanawake katika jamii.

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu unapendekeza kama ifuatavyo:

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Utafiti huu ulijikita kuchunguza dhima za nyiso za jamii ya Kiuyu Maambani. Hivyo ni wazi kwamba bado ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika nyimbo hizo. Hivyo basi, tafiti nyingi zaidi zinahitajika kufanyika zikiwa na malengo tofauti katika uwanja huu wa fasihi ya Kiswahili.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wanajamii

Kwa kutumia utafiti huu wanajamii wa Kiuyu Maambani wanaweza kuona namna jamii nyengine zinavyweza kuona nyimbo za jadi zilivyo na umuhimu mkubwa kwa jamii. Hivyo ipo haja kwa jamii hiyo kuutumia utafiti huu kama kioo cha kujirekebisha ama kuendeleza yale yanayoonekana yanafaa katika maisha ya kila siku.

## MAREJELEO

Ali, H. S. (2005). *Mafumbo Yanayopatikana katika Nyimbo za Harusi katika Ndowa za* Unguja. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar: Zanzibar.

Babbie, E. (1999). The *Basics of Social Research.* Belmont: Wardsworlth Publishing Company.

Beyanga, A. (2004). *"Taswira ya Ngombe katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Washubi"* Tasnifu ya Uzamili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Cohen, L. M. and Keith, M. (2000). *Research Methods in Education (5th edition)* London: Routledge Publishers

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press

Gitonga, N. W. (2017). *Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Juma, F. N. (2015). *Nyimbo za Harusi na Maadili ya Ndoa za Wapemba*. Tasnifu ya MA- Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

__________ (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Khatib, M. S. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mohamed, A. R. (2015). *Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Ngoma ya Msondo wa Pemba.* Tasnifu ya Uzamili ya MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mohamed, O. S. (2018). *Usasa wa Mashairi ya Nyimbo za Taarab ya Sasa: Fani na Maudhui* Tasnifu ya Uzamivu Katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mzee, A. F. (2011). *Athari za Nyimbo za taarab ya Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibar*. Dodoma: Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Muhammed, O. S. (2010). *Mchango wa Nyimbo za Unyango katika Kumkomaza Mwari Kinyumba.* Ripoti Mintarafu Wilaya ya Kinondoni nchini Tanzania. Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda. Kampala, Uganda.

Muhando, P. na Balysidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mungai, M.J. (2014). *Fani katika Nyimbo Teule za Anastacia Mukabwa.* Tasnifu ya Uzamili MA Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia Na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies: Part Two.* Nairobi: University of Nairobi.

Rashid, H. U. (2013). *Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa Jamii ya Wahiyao wa Masasi ya Lulindi.* Tasnifu ya Uzamili ya MA- Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sengo, T. S. Y. (1973). *Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii.* Jarida la Kiswahili. Dar-es Salaam: TUKI.

__________ (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIA.

Senkoro, F. E. M..K . (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TAKILUKI, (1983). *Fasihi Simulizi ya Zanzibar*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing house.

Wamitila, K. W. (2002). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Kenya Oxford University Press.

__________ (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Chuo Kikuu Dar-es-Salam.

__________ (2008). *Kanzi za Fasihi Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vde- Muwa Publishers Limited.

Waziri, M. M. (2016). *Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Singo katika Kijiji cha Uzini Zanzibar*. Tasnifua ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# VIAMBATISHO

KIAMBATANISHO NAMBA MOJA (1):

NYIMBO ZA NYISO ZA JAMII YA KIUYU MAAMBANI

1. **SIRI**

Kakae mama kakae, kakae na mumeo

Siri ya nyumba ni mbili kupata au kukosa

2. **KIGUMU**

Kigumu mwari kigumu

Kina mrema

Kina mrema aeee kina mrema

Mume ataka tunzwa kina mrema

Tena ataka kupambwa

Kina mrema

Kwa mkadi na waridi

Kina mrema aeee kina mrema.

3. **PENDO**

Ndume hio masikini,

ndume isijeihini

kukicha aenda kazini

mwana msailie pendo mwana msablilie pendo

4. **MWARI**

Mwari wangu chanjaa eee

Chanja mvua

Mwari wangu chanjaa eee

Chanja mvua

### 5. KIAZI

Kiazi mama kiazi cha nyelele

Kiazi simpi somo kiazi kinnyelele

Kina mafundo mafundo, juu kinaota nywele

### 6. RUWANJA

Mfywagirire mfywagirire ruwanja

Mwenzenu wangweta hao wakifyagira

Mfwagirire aee mfyagirire ruwanja

### 7. KIGUGUSI

Kigugusi amwambia unyayo

Ukatazwalo ndilo ufanyalo

Mgeni wetu wajana na leo kaja

### 8. WAGENI

Pano pakanja kujiri wageni

Pano pakanja kujiri wageni

Kujiri wageni kujiri wageni

### 9. KUMEKUCHA

Kumekucha eee

Kumekucha kumenanauka

Mwenye tama na atamauke

tupe mamae harusi

Tupe kinura mgongo

**10. MROMBO**

Nami ni mrombo nisingali kuja

Nami ni mrombo nisingali kuja

Ni mrombo na somo yangu

**11. MZIMU**

Sona sona sona mzimu sona

Mzimu huu wa nani

Mzimu huu wa tate

Watate wali perere

Waliperere watinya

Tulisake sake

Tulisaure saure

Nyikanga hao tuwape mbeu wapande

Nyikanga hao tuwape mbeu wapande

**12. SOMO**

Nawa nawa somo yangu nikwambie

Ikiwa kuna makosa somo nikuangukie

Kuna hadithi za wari somo nikuhadithie

Na wazee nawaee somo

Tumbo langu lina njawaa

**13. MOSI**

Mosi nataka la mosi uimosirire

Pili nataka la pili unipiririre

Tatu nataka la tatu unitaturire

Mwari wangu anandonya na uperere

**14. PAMRANGO**

Pamrango parindata ndata

Pari ndata ndata

Pamrango parindata parindata ndata

Upate ndira upite

Paripotata ritataure tataa

Paripotata ritataure tataa

Upate ndira upite

**15. KITURI**

Mwakituri eeee mwakituri  turia hapa

Mwakituri eeee mwakituri  turia  hapa

Mwakituri eeee mwakituri turia  hapa

**16. MKIA WA NG`OMBE**

Kwaja mkia wa ngombe huo

Kwaja mkia wa ngombe huo

Ukienda udama udama

Ukirudi udama udama

**17. RUGUMBA**

Rugumba  eeee

Rugumba eeee

Rugumba kamwambie runyayo

Na runyayo kamwambie sigino

Na sigino umwambie rugoti

Na rugoti umwambie rupaja

Yuwaja aeeeeyuwaja aeeee

Yuwaja mgenio yuwaja yuwaja

**Kiambatanishi Na. 2: Maswali kwa Ajili ya Kinamama Wanaozielewa Nyimbo za Nyiso za Jamii ya Kjiji cha Kiuyu Maambani.**

MADA: *Kuchunguza Dhima za Nyiso za Jamii ya Kiuyu Maambani*

Msimamizi / Mtafiti …………………….. Tarehe ………………

Maelekezo:

Kwa moyo wa upendo na huruma unaombwa kutoa ushirikiano kwa kadri uwezavyo katika kufanikisha mchakato wa utafiti huu. Maswali haya yanalenga kupata data ambazo zitafanikisha kukamilika kwa utafiti huu.

TAARIFA ZA MTAFITIWA.

1 Jina (sio lazima) ……………………………………….

Sehemu unayoishi ……………………………………

Mkoa ……………………………..

Wilaya ……………………………….

Shehia ………………………………….

Tarehe …………………………………

3 Je, umewahi kuhudhuria katika sherehe ya unyago katika kijiji cha Kiuyu Maambani Pemba?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

4. Kama ndio ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika sherehe za unyago katika kijiji cha Kiuyu Maambani Pemba?

5. Taja nyimbo zisizopungua tano

(a) ……………………………………………………………………

(b) …………………………………………………………………….

(c) ……………………………………………………………………

(d) …………………………………………………………………………….

(e) ……………………………………………………………………………..

6. Watumiaji wakuu wa nyimbo za nyiso ni akina nani?

(i) Wazee [ ] (ii) Watoto [ ] (iii) Makungwi [ ] (iv) Walimu (v) Vijana [ ]

7. (a) Jee kuna dhima zinazojitokeza katika nyimbo za nyiso?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

(b) Kama ndio, taja dhima za nyimbo za nyiso kwa vijana

(i) ………………………………. (ii) ……………………………………

(ii) ……………………………… (iii) …………………………………….

(iv) ……………………………… (v) …………………………………….

8. (a) Jee! nyimbo za nyiso zina dhamira zozote?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

(b) Kama ndio, taja dhamira hizo:

i) …………………………………………..

ii) ……………………………………………

iii) ………………………………………….

(c) Kama hapana toa sababu zako

(i)……… …………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(ii)…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(iii) …………………………………………………………………………